Nipashe
Jumatatu Novemba 4, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580066
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## ‘Elimu bure’ 485,866 wa kwanza kufanya mtihani kidato cha 4 leo

UKURASA 2




UKURASA 13

UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA:

# Wagombea wakesha siku 3 kurejesha fomu

• **Waziri** aonya watendaji waliofunga ofisi... *Endelea ukurasa 2*



## 46,000 mwaka 1 wapata mikopo

UKURASA 3

Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Kikosi Maalum cha Uhandisi cha 121KJ, kutoka Ngerengere mkoani Morogoro, wakiendelea na kazi ya kuweka daraja la muda katika Mto Nderema, wilayani Handeni, mkoani Tanga, baada ya daraja lililokuwapo kusombwa na mafuriko kutokana na mvua kubwa zilizonyesha. **PICHA: STEVEN WILLIAM**


Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

# JPM ateua mrithi wa CAG

• **Wamo** pia majaji, balozi, kamishna wa kazi...*Endelea uk.2*

**MICHEZO** KILI MARATHON YAZINDULIWA RASMI UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

## ‘Elimu bure’ kufanya Mtihani wa Taifa leo

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema kwa mara ya kwanza wanafunzi wa kidato cha nne wanaosomeshwa bure na serikali, watafanya mtihani wa kidato cha nne unaoanza leo nchini.

Waziri Jafo aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusiana na taarifa ya kuanza kwa mtihani huo.

Alisema jumla ya watahiniwa 485,866 (wavulana 229,838 na wasichana 256,028) wanatarajiwa kufanya mtihani huo.

“Napenda nitumie fursa hii kuwakumbusha Watanzania wenzangu kuwa, wanafunzi wanaoanza mitihani yao kesho (leo) ya kuhitimu kidato cha nne, walianza kidato cha kwanza Januari 2016 baada ya serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani.

“Kwa maana nyingine, hawa ndiyo wanafunzi wa awamu ya kwanza walioanza masomo yao ya kidato cha kwanza kupitia Mpango wa Elimu Msingi Bila Malipo ulioanza kutekelezwa na serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dk. John Magufuli,” alisema.

Jafo aliongeza: “Kama nilivyotangulia kusema, watahiniwa wa shule wanaotarajiwa kufanya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2019 ni 433,052 ikilinganishwa na wanafunzi waliofanya mtihani kama huo mwaka 2018, ambao walikuwa 427,181.

“Kwa sababu hiyo, mwaka huu, tuna ongezeko la wanafunzi 5,871 sawa na ongezeko la asilimia 1.37, kulinganishwa na wahitimu wa mwaka 2018.”

Waziri huyo alisema takwimu zinaonyesha idadi ya wanafunzi wanaohitimu kidato cha nne imekuwa ikiongezeka kila mwaka.

Alibainisha kuwa mwaka 2016, jumla ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kidato cha nne ilikuwa 349,524, mwaka 2017 wanafunzi 317,777, mwaka 2018 wanafunzi 427,181 na mwaka 2019 wanafunzi 433,052. Kwa sababu hiyo, kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka huu, jumla ya wanafunzi 83,528, sawa na asilimia 23.9 wameongezeka.

Alisema serikali ya awamu ya tano imeendelea kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika elimu na kwa sababu hiyo, kwa mwaka 2019/20 imetenga bajeti ya Sh. bilioni 288.485 kutekeleza Mpango wa Elimu Msingi Bila Malipo kwa wanafunzi wote kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne.

Alisema serikali itaendelea kutoa fedha ya chakula kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita kwa shule zote za umma. Alisema wanafunzi takribani milioni 12 kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita wanafaidika na mpango huo.

Alisema tangu mpango huo uanze mwaka 2016, Sh. bilioni 937.54 zimetumika kugharamia elimu ya wanafunzi hao.

“Hili ni jukumu kubwa la kupongeza kwa serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Dk. John Magufuli,” Jafo alisema.

Jafo aliwataka viongozi na watendaji wote wanaoshiriki katika usimamizi na uendeshaji wa mitihani hiyo kufanya kazi zao kwa weledi, maadili na kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za usimamizi na uendeshaji wa mitihani hiyo kama ilivyoelekezwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Alisema serikali isingependa kusikia tatizo la makusudi litakalosababishwa na wanaohusika na usimamizi na uendeshaji wa mitihani hiyo.

Jafo pia aliwataka wanafunzi kujiepusha na vitendo vya udanganyifu kwa kuwa watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

# Wagombea wakesha siku 3 kurejesha fomu

**Na Waandishi Wetu**

IKIWA imebaki siku moja kufungwa kwa uchukuaji na urejeshaji wa fomu za kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vituko vimeendelea kuripotiwa kutawala mchakato wa uchaguzi huo.

Baadhi ya vituko hivyo ni kile kilichodaiwa na uongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) baadhi ya wagombea wake wilayani Maswa mkoani Simiyu wamelazimika kukesha kwa siku tatu kwenye ofisi za serikali za mitaa za kata za Sola, Shanwa na Nyalikungu ili kurejesha fomu hizo.

Katika taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa chama hicho, Tumaini Makene, jana, ilidaiwa ofisi hizo za serikali hazijafunguliwa tangu Novemba, Mosi, mwaka huu, hivyo kusababisha wagombea kushindwa kurejesha fomu katika ofisi husika.

“Ofisi za Kata ya Sola, Shanwa na Nyalikungu wilayani Maswa hazijafunguliwa tangu Novemba Mosi, mwaka huu. Wagombea wetu wanakesha wakipelekewa chakula na maji palepale hadi fomu zipokewe,” Makene alieleza katika taarifa yake hiyo.

Kwa mujibu wa ratiba ya mchakato wa uchaguzi huo, uteuzi wa wagombea ambao hufanywa na Msimamizi wa Uchaguzi katika kata husika, unatarajiwa kufanyika kesho kwa nafasi za uenyekiti wa kijiji/mtaa, ujumbe wa halmashauri ya kijiji/mtaa kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni huku kampeni zikitarajiwa kuanza Novemba 17 hadi 23, mwaka huu.

**WAZIRI AONYA**

Akizungumzia dosari zinazoibuka katika mchakato wa uchaguzi huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliwataka wasimamizi wa uchaguzi kuhakikisha vituo vyote vinafunguliwa ili

INAENDELEA UK. 8



Mchuuzi wa pilipili akiwa amejifunika sahani ili kujikinga na jua kali, katika eneo la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JPM ateua mrithi wa CAG Assad

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amemteua Charles Kichere kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Kichere anachukuwa nafasi ya Prof. Mussa Assad ambaye kipindi chake cha miaka mitano katika nafasi hiyo kinamalizika leo.

Kabla ya uteuzi huo, Kichere alikuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, iliwataja wateule wengine kuwa ni pamoja na Katarina Revocati aliyeteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe.

Kabla ya uteuzi huo, Revocati alikuwa Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na anachukua nafasi ya Kichere ambaye ameteuliwa kuwa CAG. Rais Magufuli pia amemteua Aisha Amour kuwa Balozi wa Tanzania nchini Kuwait. Kabla ya uteuzi huo, Amour alikuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Rais pia amemteua Kanali Francis Mbindi kuwa Kamishna wa Kazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Kanali Mbindi anachukua nafasi iliyoachwa wazi na Gabriel Malata ambaye hivi karibuni aliteuliwa kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali.

Taarifa hiyo ilieleza kwa Rais Magufuli amefanya uteuzi wa majaji 12 wa Mahakama Kuu ambao ni pamoja na Dk. Zainabu Mango, Edwin Kakolaki, Dk. Deo Nangela, Fredrick Manyanda na Elizabeth Mkwizu.

Wengine ni Augustine Rwizile, Ephery Sedekia, Angaza Mwaipopo, Joachim Tiganga, Kassim Robert, Said Kalunde na Angela Bahati.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa wateule hao wote pamoja na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna watano wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambao waliteuliwa hivi karibuni, wataapishwa leo saa 3:30 asubuhi Ikulu jijini Dar es Salaam.

**MAAGIZO KWA JAFO**

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli jana alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, kufanya mabadiliko kwa Halmashauri ya Mji wa Ifakara na Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro.

Katika maagizo yake, Rais Magufuli aliagiza Halmashauri ya Mji wa Ifakara iongezwe idadi ya kata kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero.

Rais pia ameagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ibadilishwe jina na iitwe Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba. Makao Makuu yawe Mgeta kama ilivyoamuliwa na Baraza la Madiwani.

Pia amewasisitiza viongozi wa halmashauri kutowayumbisha wananchi na watumishi kuhusu utekelezaji wa maelekezo hayo.

Rais Magufuli amemwagiza Jafo kusimamia utekelezaji wa maelekezo hayo kwa mujibu wa sheria.

HABARI KITAIFA



Mdhibiti na Mkuguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, na Mwenyekiti Mtendaji wa Taasisi ya Wajibu, Ludovick Utouh (wa pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Enson Africa, Alex Kanage, wakaguzi wa mahesabu na watoa ushauri alipotembelea banda lao katika Maonyesho ya Dawati la Mhasibu lililoandaliwa na Chama cha Wahasibu (TAA), yaliyofanyika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwaka wa kwanza mikopo elimu ya juu wafika 46,000

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imetangaza orodha ya awamu ya tatu yenye jumla ya wanafunzi wa mwaka kwanza 4,785 waliopata mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 14.3.

Idadi hiyo inafanya jumla ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliopata mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 162.86 hadi sasa kufikia 46,838.

Orodha ya kwanza ilitolewa Oktoba 17, mwaka huu na ilikuwa na wanafunzi wa mwaka wa kwanza 30,675 waliopata mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 113.5.

Orodha ya pili ilitolewa Oktoba 26, mwaka huu ikiwa na wanafunzi wa mwaka wa kwanza 11,378 waliopangiwa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 35.06.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, ilieleza kuwa wanafunzi waliopata mikopo katika awamu ya tatu wanaweza kupata taarifa zao kupitia akaunti walizotumia kuomba mkopo (SIPA - Student's Individual Permanent Account).

Pamoja na SIPA, Badru alisema majina yote ya waombaji waliofanikiwa kupangiwa mikopo katika awamu hiyo ya pili yanapatikana katika mtandao wa HESLB wa uombaji mkopo (https://olas.heslb.go.tz) na tovuti ya bodi (www.heslb.go.tz).

"Awamu hii ya tatu inajumuisha wanafunzi wahitaji ambao wamekamilisha taratibu za udahili pamoja na kukamilisha marekebisho ya maombi yao yaliyokuwa na dosari. Tutaendelea kufanyia kazi maombi yanayorekebishwa na wale wenye sifa watapangiwa," Badru alisema katika taarifa yake hiyo.

Kuhusu taratibu za malipo kwa wanafunzi, Badru alisema fedha za wanafunzi waliopata mikopo zimeshapelekwa vyuoni na vyuo vimeelekezwa kuhakikisha fedha zinawafikia wanafunzi walengwa mara wanapofika na kukamilisha taratibu za usajili.

"Serikali imeshatupatia Sh. 125 bilioni ambazo tulikuwa tunazihitaji kwa ajili ya malipo ya robo ya kwanza ya Oktoba hadi Desemba mwaka huu na sisi tumeshatuma vyuoni na maofisa wetu wameanza kwenda vyuoni ili kukutana na wanafunzi na kutatua changamoto iwapo zitajitokeza," Badru alisema.

Badru aliongeza kuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020, serikali imetenga Sh. bilioni 450 kwa ajili ya jumla ya wanafunzi 128,285. Kati yao, 83,285 ni wenye mikopo wanaoendelea na masomo ya mwaka wa pili, tatu na kuendelea.

"Bodi inapenda kuwasihi waombaji wa mikopo kuwa watulivu wakati mchakato wa upangaji wa mikopo kwa wanafunzi wenye sifa kwa awamu inayofuata ukiendelea," alisema.

# CWT yatoa tahadhari udanganyifu mitihani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimewataka walimu watakaosimamia mtihani wa kidato cha nne unaoanza leo nchini, kuwa waadilifu na kujiepusha na vitendo vya udanganyifu.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa CWT, Mwalimu Deus Seif, alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini.

Mwalimu Seif alisema mtihani huo ndiyo unawaandaa wanafunzi kujiunga na kidato cha tano na vyuo mbalimbali.

Alisema ili haki itendeke, walimu ambao ndiyo maofisa wa Baraza la Mitihani (Necta) katika ngazi yao, wanatakiwa kuwa waadilifu katika kusimamia mitihani hiyo ili kuondokana na vitendo vya udanganyifu ambavyo vimekuwa vikijitokeza.

"Walimu tunatakiwa kuwa mastari wa mbele katika kuhakikisha mtihani huo unafanyika katika mazingira ya utulivu mkubwa kwa kutojihusisha na vitendo vyovyote vya udanganyifu katika maeneo yetu tunayosimamia," alisema.

Aliongeza kuwa walimu wakiwa waadilifu katika kusimamia mitihani hiyo, wataisaidia CWT kuondokana na adha ya kuingia katika migogoro ya kuwatetea walimu watakaoingia matatani kutokana na udanganyifu.

Aliwataka walimu wote nchini kubadilika kwa kuacha kujihusisha na vitendo vya udanganyifu ukiwamo wizi wa mitihani.

"Tumekuwa tukikutana na walimu lakini mara zote nawaambia walimu kuwa tunatakiwa kubadilika, sisi wenyewe kwa kuwa waadilifu katika zoezi la usimamizi wa mitihani ili kuondokana na kulindwa na Jeshi la Polisi," alisema.

Kiongozi huyo wa CWT alisema tayari wameshakutana na serikali na kujadiliana kuhusu maslahi ya walimu ambao watashiriki katika usimamizi wa mitihani.

"Oktoba 16, tulikuwa na kikao na watendaji wa serikali akiwamo Katibu Mkuu wa Baraza la Mitihani nchini na waliutuahidi hapatakuwa na changamoto yoyote ile kwani suala la usafiri, malipo pamoja na stahiki nyingine zipo tayari, labda changamoto zile ndogondogo ambazo huwa hazikosekani, lakini mambo yote yapo sawa," alisema.

# Wakala wa Serikali Mtandao waagizwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, imewaagiza Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA) kubuni njia zaidi za kurahisisha utendaji wa shughuli za serikali kwa kutumia Tehama, kwa sababu serikali inawategemea wao.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwanne Nchemba, wakati wa kikao cha pamoja cha kujadili mambo mbalimbali dhidi ya Menejimenti ya wakala kilichofanyika jijini hapa.

Mwanne alisema wakala huo wanakila sababu ya kubuni mbinu zaidi ambazo zitarahisha utendaji kazi katika maeneo mbalimbali hasa ukizingatia teknolojia ya mtandao inakua kila uchao. "Sisi kamati tunawapongeza na tunatambua jitihada mnazofanya katika kuhakikisha serikali inakuwa ya kimtandao ili kupunguza gharama za uendeshaji kwa serikali na kutoa huduma kwa umma mahali popote na kwa gharama nafuu," alisema Nchemba.

Aidha, alisema e-Ga wanastahili pongezi kwa kazi inazofanya hasa za kuhakikisha serikali inatumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yaani Tehama katika ukusanyaji mapato na kupunguza gharama za utoaji huduma kwa umma.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, aliwataka watumishi wa wakala kuongeza bidii zaidi katika kazi kwa kuwa dunia ya sasa inategemea sana Tehama katika utendaji kazi. "Tambueni kuwa Serikali Mtandao imesaidia katika ukusanyaji wa mapato serikalini na kadiri mapato yanavyoongezeka, ndivyo inavyoweza kuwahudumia wananchi kwa urahisi na kwa wakati," alisema Mkuchika.

Aidha, alisisitiza kuwa watumishi wa wakala wanatakiwa kutambua kuwa nafasi yao ni kubwa katika kufikia malengo ya wakala na azma ya serikali ya kutumia Tehama katika shughuli zake mbalimbali. Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao, Dk. Jabiri Bakari, aliiambia kamati hiyo kuwa kwa kutumia wataalamu wa ndani, wakala umetengeneza mifumo mbalimbali kama vile Mfumo wa Ukusanyaji Mapato Kielektroniki (GePG), Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office), Mfumo wa Baruapepe Serikalini (GMS), Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi (ERMS), Mfumo wa Vibali vya Kusafiri Nje ya Nchi (e-Vibali) pamoja na mifumo mingine ili kurahisisha utendaji kazi serikalini na utoaji huduma kwa umma.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi wa Uratibu wa Miundombinu ya Tehama, Benjamin Dotto, alisema kuwa wakala hiyo imeunganisha kwa data na sauti wizara, idara zinazojitegemea, wakala na mamlaka za serikali za mitaa katika mtandao mmoja wa mawasiliano wa serikali ambao ni salama na mtandao huo umeunganishwa katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Alifafanua zaidi mbele ya kamati hiyo kuwa wakala una wataalamu wa ndani wanaofuatilia mtandao huo kwa karibu na inapobainika tatizo au changamoto yoyote wataalamu hao hushughulikia kwa haraka ili kutoathiri utendaji kazi.


**MEDIA COUNCIL OF TANZANIA**

**PUBLIC NOTICE**

The President of the Media Council of Tanzania (MCT), does hereby pursuant to Article 13 of the MCT Constitution give notice to members of MCT that the 21st National General Convention (NGC) of the Media Council of Tanzania (MCT) shall be held on November 29, 2019 in Dar es Salaam at the venue to be announced.

The proposed agenda at the NGC is as follows:

1. Opening;
2. Adoption of Agenda;
3. Minutes of the 20th National General Convention held at Zanzibar Ocean View Hotel on October 05, 2018;
4. Matters Arising from the 20th NGC;
5. Report of the Executive Secretary;
6. Adoption of 2018 Audited Financial Statements;
7. Appointment of External Auditors for the period ending December 31, 2019;
8. A.O.B;
9. Closing.

MCT members who have not paid their annual subscription fees during the prescribed time are hereby reminded to do so promptly.

Judge Thomas B. Mihayo
President
Media Council of Tanzania (MCT)

HABARI KITAIFA

# Maelfu wanafunzi mikoa 3 wapewa elimu ya viwango

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WANAFUNZI 10,757 kutoka shule tisa za sekondari na msingi katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Pwani, wamepatiwa elimu ya viwango iliyotolewa na maofisa wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) itakayowasaidia kuwa mabalozi wa viwango.

Maofisa hao walitoa elimu hiyo wiki iliyopita kwenye mikoa hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Viwango yaliyoadhimishwa na shirika hilo kuanzia Oktoba 21, hadi 31, mwaka huu.

Akizungumza kuhusu mafunzo hayo mkoani Morogoro, Ofisa Uhusiano wa shirika hilo, Neema Mtemvu, alisema walitumia maadhimisho hayo kutoa elimu kwa wanafunzi hao kuhusiana na majukumu ya shirika.

Alisema pia walitoa mafunzo ili wanafunzi hao watambue umuhimu wa viwango, madhara ya kutumia bidhaa zisizokidhi viwango na sababu za maadhimisho ya Siku ya Viwango Duniani.

Mtemvu, aliwataka wanafunzi hao

INAENDELEA UK. 8



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Shinyanga, Antony Gwandu, akitoa mafunzo kwa waendesha bajaji na pikipiki kuhusa jinsi gani wanatakiwa kuvaa wakiwa kwenye chombo cha moto, na sio kama alivyovaa kijana (pichani), wakati wa kikao cha utambulisho wa viongozi wa mkoa huo wa chama cha wamiliki na waendesha daladala za pikipiki. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Onyo wahitimu vyuo vikuu kung'ang'ania ajira za serikali

Distributed via ippmedia

**Na Moshi Lusonzo**

VIJANA wanaohitimu masomo ngazi ya vyuo vikuu wametakiwa kuacha kung'ang'ania ajira za serikali, badala yake watumie fursa wanazopata kujiajiri katika ujasiriamali.

Wito huo umetolewa jijini Dar es Salaam jana na Katibu wa Baraza la Taifa la Uwekezeaji la Wananchi Kiuchumi, Meng'i Issa, wakati akifunga mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana 100 yaliyoandaliwa na Taasisi ya An Nahl Trust.

Alisema wakati wa kusoma kwa niaba ya kupata ajira serikalini umepita kwani idadi kubwa ya wahitimu ni kubwa kuliko nafasi zinazotakiwa kujazwa.

"Zamani ilikuwa rahisi kwa mtu anayemaliza elimu ya chuo kupata ajira serikalini, lakini kwa hivi sasa ni vigumu wanaajiriwa idadi ndogo ambao wanakidhi vigezo. Nawashauri wakati mnachukua masomo yenu hakikisheni mnaangalia fursa zingine ili mtakapomaliza mjiajiri wenyewe," alisema Beng'i.

Katibu huyo alisema tatizo la uhaba wa nafasi za kazi halipo serikalini pekee, hata katika sekta binafsi wasomi wanaoajiriwa ni wachache kutokana na kukosa vigezo vinavyokubalika ikiwamo kushindwa kujieleza na uzoefu wa kazi.

"Hakuna sehemu ambayo vijana wanaweza kupata ajira kwa kiwango kikubwa, lazima tuwaeleze na kuwapa mafunzo ambayo wao wenyewe wanaweza kuyatumia kwa kuanzisha miradi yao ya kibiashara ambayo itawaingizia kipato na kuajiri watu wengine," aliongeza kusema.

Pia amepongeza Taasisi ya An Nahl kwa kushirikiana na Mfuko wa Nama wa Malaysia kwa kutoa mafunzo ambayo yatawasaidia vijana hao kutumia fursa zinazowazunguka kubuni miradi na kuiendesha kiufanisi.

Mratibu wa mafunzo hayo, Shabani Mlongakweli, alisema mafunzo hayo ya siku nne yaliwahusisha vijana wahitimu wa ngazi ya shahada na stashahada kutoka vyuo mbalimbali nchini. Alisema kwenye mafunzo hayo, wamepewa mbinu mbalimbali za namna ya uendeshaji wa biashara na kupata kipato halali, kujitangaza pamoja na matumizi ya mitandao kutafuta fursa za kiuchumi.






# 95,000 washindwa kuhuisha uanachama Bima Afya Jamii

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANACHAMA 95,489 wa mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii CHF iliyoboreshwa mkoani Shinyanga, wametajwa kushindwa kuhuisha uanachama wao, kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo hali ya kiuchumi na walioku-wa wakilipiwa na mashirika baada ya kusitisha huduma hiyo wakakosa fedha za kulipa.

Hayo yalibainishwa juzi na Mratibu wa CHF mkoani Shinyanga, Lidya Kwesigabo, kwenye kikao na maofisa uandikishaji CHF kutoka Halmashauri za Wilaya ya Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga pamoja na Benki ya NMB, kilichokuwa na lengo la kuhamasisha uandikishaji CHF ili kuongeza wanachama.

Alisema Mkoa wa Shinyanga ulianza kuandikisha wanachama wa CHF mwaka 2016, na hadi kufikia Oktoba 2019, wana jumla ya wanachama 108,639, na kaya ambazo wameshindwa kuhuisha uanachama wao ni 95,489, na kusababisha kubaki na wanachama hai 13,150.

"Kutokana na kuwapo na kasi ndogo ya uandikishaji wanachama wapya kujiunga na CHF, pamoja na kushindwa kuzitembelea

INAENDELEA UK. 8

# Wanawake waishio na VVU waiomba serikali

**Na Rose Jacob,** MWANZA

ZAIDI ya wanawake 50 waishio na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi, wameiomba serikali kuwaangalia dhidi ya maamuzi katika familia, kutokana na kunyimwa haki ya kutoa maamuzi.

Wamedai kuwa hali hiyo inawafanya wajikute wakiathirika kisaikolojia na kusababisha wengi wao kupoteza maisha kwa msongo wa mawazo.

Hayo yamebainishwa na washiriki wa semina ya kuwajengea uwezo wanawake waishio na VVU kutoka katika mikoa ya Kanda ya Ziwa ya Mwanza, Kagera, Geita, Mara na Shinyanga iliyoandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa Kitengo cha Wanawake-UN Women kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS). "Mimi nimeanza kutumia dawa za kufubaza makali ya Virusi vya Ukimwi tangu mwaka 2002 hadi sasa, lakini sisi wanawake tunaoishi na maambukizi tunapata manyanyaso ya kutokushirikishwa katika maamuzi ya kifamilia, hivyo tunaiomba serikali itutambue na kutusaidia nasi kuwa na haki kama binadamu wengine ya kutoa mawazo maoni na kuamua jambo," alisema Hawa Ramadhani, mkazi wa Misungwi mkoani Mwanza.

Akizungumza katika mafunzo hayo ya wiki moja yaliyofanyika jijini Mwanza, Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Wanawake waishio na Virusi vya Ukimwi Tanzania, Joan Chamungu, ambaye ndiye mwezeshaji katika warsha hiyo, alisema, lengo kubwa ni kuwajengea uwezo wanawake waishio na VVU wa kukabiliana na maambukizi mapya.

"Tunawajengea uwezo wanawake waishio na maambukizi ya Ukimwi ya kuwa na mbinu za kukabiliana na unyanyapaa, ukatili wa kijinsia na kuzikwepa mila na destuli potofu ambazo zimeonekana kuwa ndio kichocheo kikubwa cha maambukizi ya Ukimwi," alisema Chamungu.

Aidha, Chamungu alisema wanaendelea na utambuzi na kuzichambua mila na destuli potofu, ili kuona wanawezaje kuisaidia jamii na wanawake waishio na maambukizi, ili wasiweze kuathirika zaidi, maana wameona wafanye hiyo kutokana na mila na desturi haziwezi kubadilishwa mara moja.

"Tunatafuta njia ambayo tunaweza kuihusisha jamii kupitia taarifa sahihi, kuweleza madhara ya mila hizo ili waweze kujua namna ya kondokana na changamoto zilizopitwa na wakati, kwa kufanya marekebisho kwa kushirikiana na wanawake hao walioshapata mafunzo husika," alisema Chamungu.

Naye Jacob Kayombo, Ofisa Msaidizi wa Programu wa UN Women Tanzania, alisema lengo kuu la shirika hilo kwa kushirikiana na TACAIDS, ni kuhimiza usawa wa kijinsia kwa kuwajengea uwezo kinamama waishio na VVU.

"Kwa kufanya jitihada za kuunda vikundi ili kuwakutanisha kwa pamoja na kuimarisha mitandao yao kwa kuhimizana wao kwa wao katika kufikia huduma ya kupata dawa za VVU na Ukimwi, maana taarifa za TACAIDS zinaonyesha kiwango cha maambukizi, vifo na unyanyapaa kwa kinamama ni mara mbili zaidi ya wanaume," alisema Kayombo.

# Magereza Simiyu kulima pamba

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, amelitaka Jeshi la Magereza kutumia jumla ya ekari 3,071,000 zilizopo mkoani hapa kwa kilimo cha pamba ukiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli la kutaka jeshi hilo kubadilika na kuingia kwenye mfumo wa uzalishaji ili liweze kuondokana na mfumo wa kutegemea bajeti kuu ya serikali kulisha wafungwa.

Ameyasema hayo wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Yusuf Masauni, mkoani hapo kwa ajili ya ukaguzi wa shughuli za taasisi zilizopo chini ya wizara hiyo pamoja na kuangalia fursa zinazopatikana katika mikoa mbalimbali nchini ili kulibadilisha Jeshi la Magereza.

"Mheshimiwa Naibu Waziri, sisi kama mkoa tuko tayari kushikana na Jeshi la Magereza kwani kuna ardhi ya kutosha na maombi nikuhakikishie hawa wakilima pamba japo ekari 100 tu na zikauzwa wataweza kufanya mambo mengi ya maendeleo ikiwamo kujenga nyumba za kuishi askari, ambazo zitakua ni za kiwango cha juu," alisema Mtaka.

Akizungumza katika ziara hiyo, Masauni alisema serikali imelipokea jambo hilo kwani ndio lengo hasa lake kuona Jeshi la Magereza linajitegemea katika uendeshaji wake pasipo kutegemea bajeti kuu ya serikali.

"Mheshimiwa Rais alishatuagiza tulibadilishe Jeshi la Magereza na tayari tushaanza na tumetenga Magereza kumi ya kimkakati nchini, ambayo yameteuliwa kuleta mapinduzi katika jeshi... ziara hii ni kuona fursa zilizopo katika mikoa mingine kupitia magereza, nakuahidi jambo hilo tumelichukua kama wizara na muda si mrefu litapatiwa ufumbuzi," alisema Masauni.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUHAMISHA SHUGHULI KWA BAADHI YA OFISI ZA TRA JIJINI DAR ES SALAAM

**Dar es Salaam, 3 Novemba 2019:**

**Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuutangazia umma kuwa, kuanzia tarehe 4 Novemba, 2019 baadhi ya ofisi za TRA za jijini Dar es Salaam zitahamisha shughuli zake kama jedwali linavyoonesha;-**

| NA | OFISI | ILIPOKUWA | ILIPOHAMIA |
|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Walipakodi Wakubwa | Mapato House (Long Room) | Wizara ya Fedha na Mipango (Mtaa wa Madaraka) |
| 2 | TRA Mkoa wa Kikodi wa Ilala | Summit Tower/Kipata – Mnazi Mmoja | Mapato House (Long Room) |
| 3 | TRA– Shauri Moyo | Mariam Tower | Mapato House (Long Room) |
| 4 | TRA Upanga | Samora House | Mapato House (Long Room) |
| 5 | TRA Mkoa wa Kikodi Kariakoo | 14 Rays Building-Gerezani | Mtaa wa Kipata Mnazi Mmoja |

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa kupiga simu bure namba 0800 780 078 au 0800 750 075 au tuma ujumbe kwa WhastsAp 0744 233 333, barua pepe huduma@tra.go.tz

**Imetolewa na**

***Richard M. Kayombo***
***KAIMU MKURUGENZI WA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI***

215497602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga zikiepuka haya, zitafanikiwa Caf

**HATIMAYE** mashabiki wa soka nchini wameshuhudia msimu mbaya kwa timu za Tanzania kuvurunda kwenye michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, Simba, Yanga na KMKM zote zimefanya vibaya kwenye Ligi ya Mabingwa wakati Azam, KMC na Malindi zikivurunda Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo, Yanga yenyewe ilijitahidi na kupenya raundi ya kwanza kabla ya kuangukia mechi ya mchujo kuwania kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika ambapo ilikutana na Pyramids FC ya Misri jana usiku.

Licha ya kuangukia kwenye mechi hiyo ya mchujo hapakuwa na matumaini ya wawakilishi hao pekee wa Tanzania kimataifa kusonga mbele baada ya mechi ya awali, Yanga kukubali kipigo cha mabao 2-1 nyumbani katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Na jana ilishuka dimbani nchini Misri kurudiana na Pyramids, lakini kukiwa na kukatishwa tamaa kwingi kutokana na Kocha Mkuu wa Yanga, Mkongomani Mwinyi Zahera kuwa wa kwanza kukata tamaa.

Zahera aliwakatisha tamaa mashabiki, wanachama wa Yanga na Watanzania kwa ujumla baada ya kueleza hakuna mchezaji hata mmoja wa timu yake anayeweza kufananishwa kwa ubora na wale wa Pyramids. Lakini akaenda mbali zaidi kwa kueleza uwezo Yanga ni wakushindana na timu kutoka nchi kama Burundi na kwamba Pyramids ni ya kiwango cha juu sana kwao.

Hakuishia hapo, kwani alifafanua zaidi kwamba wachezaji aliowasajili walikuwa ni kwa ajili michuano ya Ligi Kuu na si mechi za kimataifa kwa kuwa Yanga ilishtukizwa kushiriki michuano hiyo.

Tayari mashabiki, wanachama na baadhi ya viongozi wa klabu hiyo wanataka Zahera atimuliwe kutokana na timu hiyo kuonyesha kiwango kibovu huku hadi sasa ikishindwa kuwa na muunganiko mzuri.

Lakini pia akitupiwa lawama kwa kauli yake hiyo wakati pia yeye akihusika katika usajili wa wachezaji kwa zaidi ya asili 90, jambo ambalo ni nadra sana kwa klabu mbili kongwe Simba na Yanga kuona kocha akihusishwa kwa kiwango kikubwa kama hicho katika usajili.

Ni kweli Zahera kama kocha amekosea kutoa kauli kama hizo wakati yeye akiwa kama 'Amiri Jeshi Mkuu' hakupaswa kuwa wa kwanza kukata tamaa wakati ana kazi kubwa ya kuliongoza jeshi lake vitani.

Lakini sisi tunaamini pamoja na kubebeshwa lawama hizo, huu ni wakati wa klabu za Tanzania kujifunza kwa kuwa makini na aina ya makocha wanaowaajiri, lakini pia wachezaji wanaowasajili ikiwa ni pamoja na kuwa na timu ya muda mrefu.

Tunaamini mafanikio iliyoyapata Simba msimu uliopita kwa kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ilichangiwa pia na kikosi chao kukaa kwa pamoja muda mrefu, lakini kitendo cha msimu huu kufanya mabadiliko makubwa ya wachezaji kukawagharimu hali inayoikumba Yanga kufuatia kikosi chao kuwa na nyota wengi wapya.

Hivyo, hakuna haja ya kunyosheana vidole kwa sasa, bali klabu hizo zinapaswa kubadili sera zao za kubomoa kikosi kila msimu kwa kuwa na utamaduni wakuongeza wachezaji wasiozidi wanne ili kuwa rahisi kuzoena mapema kabla ya msimu kuanza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hili la wachezaji wa Alliance Bodi ya Ligi isimung'unye kushusha rungu

Na Adam Fungamwango

**SIKUAMINI** macho yangu kama nilikuwa naangalia moja kati ya Ligi Kuu kubwa kabisa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Ilikuwa kama naangalia mechi za mchangani maarufu kama ndondo ambazo nazo siku hizi mashabiki na wachezaji wake wameshaanza kustaharabika.

Ilikuwa ni jioni ya Alhamisi 31, Oktoba, kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza kwenye mechi kati ya Alliance dhidi ya Mbeya City.

Mchezaji Israel Patrick alipata kadi nyekundu ya moja kwa moja baada ya kufanya faulo ya ajabu kwa kumshika sehemu nyeti mchezaji mmoja wa Mbeya City.

Wakati mashabiki wote uwanjani na wale waliokuwa wakiangalia soka kwenye televisheni wakijadili tukio hilo, wengine wakitafakari, dakika ya 71, kipa wa Alliance John Mwenda naye akafanya kituko cha ajabu.

Alimkata mtama mchezaji mmoja wa Mbeya City akiwa hana mpira. Naye pia akaonyeshwa kadi nyekundu. Ilikuwa ni moja kati ya mechi iliyojaa utovu wa nidhamu wa hali ya juu kwa wachezaji wa Alliance.

Kwanza kabisa katika hili napenda kumpongeza mwamuzi wa mechi hiyo, Shomari Lawi ambaye aliwaonyesha kadi nyekundu za moja kwa moja wachezaji hao bila kupepesa macho. Labda kwa kuwa haikuwa mechi inayozihusu timu kubwa. Alifanya kazi yake vizuri.

Tukio hili likanikumbusha mechi kati ya Kagera Sugar dhidi ya Simba, mchezaji Zawadi Mauya alipomkata mtama mara tatu mchezaji wa Simba, Ibrahim Ajibu, ingawa yeye hakupewa kadi nyekundu.

Nikawa najiuliza kama baadhi ya wachezaji hapa nchini wanachukulia kuwa soka ni kazi au sehemu ya kwenda kutuliza matatizo yao kichwani. Kwa siku za karibuni kumekuwa na rafu za ajabu ambazo si za kimpira kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ninavyojua kuwa wakati mchezaji anacheza soka, pia awe analinda afya ya mchezaji mwingine kwa kutomchezea madhambi ambayo si ya kiungwana wala ya kimichezo yanayoweza kuhitimisha wasifu wake kisoka.

Lakini ninavyoona kuna baadhi ya wachezaji wa Kibongo hawajui hilo. Na kwa bahati mbaya hakuna hatua zozote za makusudi zinazofanya na Bodi ya Ligi ili kumaliza tatizo hilo.

Nilisema huko nyuma kuwa kitendo cha Bodi ya Ligi kutoa onyo tu kwa mchezaji Zawadi Mauya, basi kinaweza kufungua milango kwa wachezaji wengine kufanya uhuni kama wachezaji hao wa Alliance walivyofanya.

Kama Bodi ya Ligi ingetoa adhabu stahiki, sidhani kama kuna mtu angerudia na Zawadi angekuwa kama mfano kwa wachezaji wengine. Na kama Bodi ya Ligi ikiendelea na hili la wachezaji hawa kulifumbia macho na kutoa onyo, basi itegemee kuna baadhi ya wachezaji wataendelea na tabia hiyo wakiona hakuna chochote watakachofanywa. Mbele ya safari hatuombei, tunaweza kuona wachezaji wakichezeana rafu za kuvunjana miguu. Hivi mpaka tufike huko ndipo Bodi ya Ligi ikae na kutoa adhabu kali wakati tayari kuna mchezaji au wachezaji wameshavunjika au kuwa walemavu wa viungo na kukatisha ndoto zao kwenye soka?

Inabidi sasa Bodi ya Ligi iamke na kusawazisha mambo ili kuifanya Ligi ya Tanzania kuheshimika na kuvutia watu ndani na nje ya nchi, isionekana kama ni ligi ya mtaani kwa wachezaji kucheza kimtaani bila kufanya kitu.

Wachezaji wa aina hii ndiyo wanaosababisha kudharaulika kwa ligi kiasi cha kuwafanya baadhi ya wadhamini kukimbia kuwekeza kwenye soka kwa kuona kuwa soka ni mchezo wa kihuni.

Bodi ya Ligi iige kwa wenzao ambao hata siku moja hawakubali mchezaji yeyote kufanya uhuni au kucheza kihuni, badala yake wanataka wachezaji wenye vipaji na wenye kuonyesha uwezo wao uwanjani kwa ajili ya kuvutia wawekezaji na ndiyo maana ligi zao zinaheshimika na zina pesa.

Natarajia Bodi ya Ligi itafanya kitu kwa wachezaji hawa wa Alliance watovu wa nidhamu ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia kama hizo na wanaotaka kuiga.

# Waziri asisitiza malipo kidigitali

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amewataka wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha malipo yanafanyika kwa mfumo wa kidigitali ili kuimarisha makusanyo ya serikali.

Vilevile, amesema atafungua dawati maalum kwa ajili ya kupitia kero za malipo, ili kuwaona wakurugenzi ambao hawaendi na kasi ya mfumo huo.

Jafo aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozindua huduma ya malipo kwa M-Pesa kwenda halmashauri na manispaa mbalimbali nchini.

Kampuni ya Vodacom Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Tamisemi, ndiyo imefanikisha kuimarisha mfumo wa malipo ya kifedha kwa kusogeza huduma ya malipo kwa M-Pesa kwa ofisi zaidi ya 127 za serikali za mitaa nchini.

Waziri huyo aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kujipanga kwenda kwa kasi na malipo kufanyika kwa namba ya malipo ya serikali na siyo vinginevyo.

Alisema watu wamezoea utaratibu wa kubeba maburungutu ya fedha na kwenda kulipa, jambo ambalo linasababisha kupoteza fedha na utaratibu huo ni hatarishi.

"Utaratibu huu utasaidia kuondoa wizi au ushawishi wa watu kuiba, utakuta watu wanakimbizana na watu kupeleka benki kulipa mapato," alisema.

Alisema ukusanyaji wa malipo katika serikali ya mitaa kwa M-Pesa utasaidia kuongezeka mapato ya serikali, akidokeza kuwa mfumo huo unamshawishi mtu kufanya malipo yoyote hata akiwa amelala kitandani.

"Natamani kila wizara itumie mfumo huu. Tumepoteza fedha nyingi kwa utaratibu huu wa kuandika risiti za mikono, naamini kama wizara itatumia mifumo ya didigitali, itasaidia sana nchi yetu kusonga mbele," alisema.

"Nitafungua dawati maalum la kupitia kero mbalimbali za malipo, lengo kubwa ni kuwaona wakurugenzi ambao hawaendani na kasi," alisema. "Tuachane na biashara ya kubeba manoti, tutumie mitandao yetu ya kidigitali kufanya malipo, hakuna sababu ya kujaza noti mfukoni mpaka unaonekana kama una majipu, huu mfumo utasaidia kujiepusha na wizi hata watengenezaji wa noti bandia watazikosa hizo fedha," alisema.

Mkurugenzi wa Huduma ya M-Pesa, Epimack Mbeteni, alisema kupitia M-Pesa, Vodacom inategemea kuzifikia taasisi nyingi za serikali na binafsi ili kuwezesha mfumo wa malipo kuwa rahisi, fanisi na salama zaidi.

"Asilimia kubwa ya Watanzania wanatumia M-Pesa kufanya miamala mbalimbali kama Luku, bili za maji, faini za barabarani, ndiyo maana tukaona fursa kubwa ya kurahisisha malipo kwa serikali za mitaa kutumia M-Pesa," alisema.

Alisema ushirikiano huu na Tamisemi ni kwamba M-Pesa itawawezesha wateja wa mtandao wa Vodacom kufanya zaidi ya malipo 205 ya serikali za mitaa kwa urahisi na usalama zaidi.

Aliyataja malipo hayo kuwa ni pamoja na leseni za biashara, vibali vya ujenzi, malipo ya maegesho na huduma nyinginezo.



Wahandisi wa umeme wanawake kundi la kwanza wakipata maelezo kutoka kwa mtaalamu wa matengenezo ya umeme bila kuzima, Donald Mwakamele, ili wakihitimu waanze kufanya kazi hiyo katika maeneo mbalimbali nchini. Habari Uk. 26. **PICHA: IDDA MUSHI**

# 95,000 washindwa kuhuisha uanachama Bima Afya Jamii

**INATOKA UK. 4**

kaya ambazo zimeshindwa kuhuisha uanachama wao, tumeanzisha programu ya kutoa zawadi za pikipiki, na baiskeli, kwa maofisa ambao wataandikisha kaya nyingi," alisema Kwisegabo.

Naye Mratibu Msaidizi wa CHF iliyoboreshwa mkoani Shinyanga, Tedyson Ngware, alisema wameamua kutoa motisha hiyo kwa maofisa uandikishaji, ili wapate kutembelea kaya nyingi na kutoa elimu ya umuhimu wa kuwa na bima, ili wapate kuwa na wanachama wengi kama zamani.

Aidha, alisema Mkoa wa Shinyanga ulikuwa unaongoza kitaifa katika uandikishaji wanachama wa CHF asilimia 11.9, lakini hadi kufikia Juni mwaka huu 2019, wameshuka hadi asilimia 5, kutokana na kuwapo na kasi ndogo ya uandikishaji, huku wanachama wengine wakikosa pesa za kuhuisha uanachama wao.

Nao baadhi ya maofisa uandikishaji wa CHF iliyoboreshwa akiwamo Daudi Joseph kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, walisema changamoto kubwa ambayo wanakabiliana nayo kushindwa kuandikisha wanachama wengi ni kaya nyingi kuyumba kiuchumi.

Ofisa kutoka Benki ya NMB Tawi la Manonga Shinyanga Mjini, Timotheo Elias, alisema wameamua kufadhili utoaji wa baiskeli na pikipiki, kwa maofisa ambao wataandikisha kaya nyingi kujiunga na CHF, ili kuunga juhudi za serikali katika kuhakikisha wananchi wake wanakuwa na afya njema.

## Maelfu wanafunzi mikoa 3 wapewa elimu ya viwango

**INATOKA UK. 4**

kuhakikisha wanakuwa mabalozi wazuri ndani ya jamii kwa kuhakikisha wanatumia bidhaa zenye nembo ya ubora, kwani bidhaa zisizo na viwango zina madhara makubwa kiafya.

"Mnatakiwa kuwa makini na kuhakikisha mnachunguza bidhaa kabla hamjanunua ili kujiridhisha kama zina alama ya ubora, kwani kufanya hivyo kutawasaidia kujiepusha na madhara yatokanayo na bidhaa zisizokuwa na viwango," alisema. Alisema kuna madhara mengi yatokanayo na bidhaa zisizokuwa na viwango, zikiwamo za kiafya.

Kwa mujibu wa Mtemvu, wanafunzi waliopata elimu hiyo waliahidi kuwa mabalozi kwa kuhakikisha bidhaa zinazonunuliwa na wazazi na watu wengine ni zile zinazokidhi viwango. Wakati wa mafunzo hayo wanafunzi hao walikuwa wakiulizwa maswali mbalimbali kuhusiana na viwango na waliofanywa vizuri walipewa zawadi za aina mbalimbali za vifaa vya shule ikiwamo daftari na mabegi.

Maadhimisho hayo huadhimishwa na Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO) kila mwaka ifikapo Oktoba 14, TBS ni mwanachama.

Lakini kwa Tanzania kutokana na wiki hiyo kuangukia tarehe ya kumbukizi ya kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, TBS ilisogeza mbele maadhimisho hayo hadi kuanzia Oktoba 21 na Oktoba 31, mwaka huu.

Shule ambazo wanafunzi wake walipatiwa elimu hiyo kwa mkoa wa Morogoro ni Kayenzi, Kilakala, Kihonda, Chief Albert, Mwere A, Bungo, shule za mkoa wa Pwani ni Bundikani na Maendeleo, kwa Dar es Salaam elimu hiyo ilitolewa katika Shule ya Kibasila.

# Wagombea wakesha siku 3 kurejesha fomu

**INATOKA UK. 2**

wananchi wachukue na kurejesha fomu.

Vilevile, waziri huyo aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa hawataongeza muda wa kuchukua fomu, hivyo wananchi watumie vizuri muda uliobaki.

"Natambua kuna changamoto (matatizo) mbalimbali zimejitokeza, kuna maeneo tumeambiwa ofisi zilifungwa na tumetoa maelekezo ofisi zote zifunguliwe na watu wachukue fomu na kuzirejesha," Jafo alisema.

Alisema malalamiko yote ambayo yametokea katika maeneo mbalimbali baada ya kuyapokea alikuwa anatoa maelekezo ili kusiwapo na ukwamishaji wa mchakato wa kuchukua fomu.

"Wale niliowapa dhamana, niwaagize wasimamizi wote wa uchaguzi kuhakikisha vituo vyote vinafunguliwa kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria zetu," Jafo aliagiza.

Waziri huyo alisema hataki kuona mtu anabughuziwa kwa jambo lolote, hivyo kila mmoja ni ruksa kurejesha fomu ama kuchukua fomu bila kuwapo kwa vikwazo.

"Niwaombe wadau wengine, kuna maeneo mengine kama Mkoa wa Mbeya, nilipokea taarifa ya kufungwa ofisi nikatoa maelekezo, kumbe kuna watu wanamtishia msimamizi wa uchaguzi, naye anagoma kutokana na kutumiwa 'message' (ujumbe) za vitisho," alisema.

"Wadau tuache kuhujumiana kwa njia moja au nyingine kwa sababu hujuma hizi inawezekana kwamba zinatoka katika maeneo mbalimbali, lakini maeneo mengi yameenda vizuri, sehemu chache zimekuwa na malalamiko. Kwa mfano, nimepata kesi kule Kigoma, hii haina maana kwamba tunatafuta mchawi."

Jafo aliwataka wasimamizi wa uchaguzi 184 kuhakikisha vituo vyote vinafunguliwa ili watu wachukue na kurejesha fomu.

"Tuendelee kushiriki katika uchaguzi huu kwa amani na wakuu wa mikoa na wilaya kuendelea kusimamia suala zima la amani," alisema.

"Kama kuna mtu sijui anazuiliwa, aende Jeshi la Polisi wasimamie, kazi yao ni kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri na kama kuna vizuizi, ni vizuri taarifa ikafika katika vyombo vyetu vya usalama.

"Zile kasoro ambazo zimejitokeza hapa na pale nimeagiza kurekebishwa, hizo changamoto (matatizo), hatutaki kusikia makandokando yoyote, huu uchaguzi ndiyo unatengeneza msingi wa uchaguzi mkuu ujao."

Uchaguzi huo uliopangwa kufanyika siku 20 zijazo, unatarajiwa kuhusisha wapigakura milioni 19.7 nchi nzima, ikiwa ni ongezeko la takriban watu milioni nane kulinganisha na waliojiandikisha mwaka 2014 ambao walikuwa 11,882,086.

**Imeandikwa na Beatrice Shayo na Enock Charles**



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Stella Ikupa (katikati), akikata utepe kuzindua soko kwa ajili ya kuuzia bidhaa za wajasiriamali zinazotengenezwa na makundi maalumu ya walemavu, lililopo Kata ya Buigiri, wilayani Chamwino, Mkoa wa Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Bil. 23.5/- sasa zaokolewa kwa umeme wa gridi kufika kusini

**Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme la Taifa (Tanesco), limesema kwamba taifa linaokoa wastani wa Sh. bilioni 23.5 kila mwaka kwa sababu umeme kutoka gridi ya taifa umeanza kusambazwa mikoa ya kusini.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari, juu ya mafanikio kuhusu programu ya miaka minne ya usambazaji wa nishati ya umeme nchini, Meneja Uhusiano wa Tanesco, Leila Muhaji, aliwashukuru wananchi na viongozi mikoa ya kusini kwa ushirikiano walitoa kwa wahandisi na wafanyakazi wengine wa Tanesco ambao wameshiriki katika zoezi hilo. "Fedha zilizookolewa zimeweza kutumika kuiendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na lengo likiwa kila Mtanzania afikiwe na umeme popote alipo," alisema.

Alitaja vituo ambako generetaza dizeli zimezimwa baada ya kuunganishwa na umeme wa gridi ya taifa kuwa ni Songea, Mbinga, Namtumbo, Madaba na Liwale.

"Tunayo furaha kueleza taifa kwamba katika kutekeleza programu ya miaka minne ya usambazaji wa nishati ya umeme tumepata mafanikio makubwa sana. Sasa serikali inaokoa wastani wa Sh. bilioni 23.5 kwa mwaka kwa sababu tumezima mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta katika vituo vyetu vya Songea, Mbinga, Namtumbo, Madaba and Liwale," alieleza meneja huyo na kuongeza kwamba shirika limetiwa moyo na mafanikio hayo kwa sababu yametokana na bidii na kujitolea kwa wafanyakazi wake.

Usambazaji wa nyaya za umeme wa gridi unahusisha kuweka nguzo za miti na za vyuma hata katika maeneo ya hatari kwani umeme unapita katika mbuga, juu ya mito, mabonde, mistitu na milima.

Usambazaji wa umeme chini ya mpango wa miaka minne uliobuniwa na Tanesco ni sehemu ya mchango wa shirika hilo katika kutekeleza mpango wa kitaifa wa 'kukazania utoaji huduma katika maeneo sita ya kipaumbele' yaliyoainishwa katika mwaka wa fedha 2012/13. Maeneo hayo ni nishati na gasi asilia, kilimo, maji, elimu, usafiri na ukusanyaji mzuri wa raslimali za taifa.

Maeneo hayo yalitamkwa wakati wa kuzindua mpango wa taifa wa 'Matokeo Makubwa Sasa' mwaka huo wa fedha.

# Wapewa angalizo udanganyifu wa mitihani

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KATIBU Tawala Wilaya ya Wete, Mkufu Faki Ali, amewataka wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mitihani yao ya taifa kuacha tabia ya udanganyifu kwani unaleta athari kwao pamoja na taifa kwa ujumla.

Alisema wanafunzi wengi wamekuwa wakishindwa kufanya mitihani yao kwa uwezo wao na badala yake wamekuwa wakijihusisha na udanganyifu, jambo ambalo ni hatari kwao.

Aliyasema hayo katika Shule ya Sekondari Mchangamdogo alipokuwa akizungumza na wanafunzi wa kidato cha nne ambao wanatarajiwa kufanya mitihani ya kitaifa leo.

Alieleza kuwa shule hiyo imekuwa na sifa ya kufaulisha wanafunzi wengi kila mwaka, hivyo aliwaomba wanafunzi hao kulinda historia hiyo pamoja na kuwasisitiza kuthamini juhudi zinazotolewa na walimu wao.

Katibu huyo aliwaomba wanafunzi hao kutumia muda wao vizuri wakati wa mitihani yao kwani kuna baadhi yao wanachelewa katika vituo vyao vya kufanyia mtihani, hivyo kukosa kufanya mtihani. "Niwaombe wanafunzi wangu kuuthamini sana muda ambao tumepangiwa kufanya mitihani yetu, vinginevyo tutakosa kufanya mtihani ikiwa tutachelewa kufika mapema katika vituo vyetu," alisema Mkufu.

Aliwaambia wanafunzi hao kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejitahidi vya kutosha katika kuweka misingi mizuri katika sekta ya elimu nchini. Akitoa wito kwa wanafunzi hao kujiepusha na vitendo vya udhalilishaji wanapokuwa majumbani kwao. "Lakini huku tukiwa tunasubiri matokeo yetu tujiendeleze kwa fani mbalimbali ambazo zitaweza kutusaidia katika maisha yetu pamoja na kujiunga katika vikundi vya ujasiriamali," alieleza Mkufu. Naye Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Wete, Riziki Makame Faki, aliwataka wanafunzi hao kujiamini wakati wa kufanya mitihani yao.

# RC ashangaa matokeo mabaya

**Na Idda Mushi,** ULANGA

PAMOJA na serikali kuwathamini wananchi wa Ulanga na kutoa Sh. milioni 860 kwa Sekondari ya Wavulana Kwiro kusaidia ukarabati wa mabweni na madarasa, bado shule hiyo imeendelea kuwa na matokeo yasiyoridhisha ikilinganishwa na shule nyingine ambazo zina hali ngumu na ziko kwenye mazingira magumu ambazo zinafanya vizuri kitaifa.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, amesema hayo baada ya kutembelea shule hiyo katika ziara ya kushtukiza, alipofika kujitambulisha wilayani humo.

Alisema licha ya kazi ya ukarabati unaoendelea kuonena ni nzuri, bado anahitaji kufahamu matumizi ya fedha za ukarabati na mabadiliko kwenye kiwango cha ufaulu hasa kuanzia mtihani ujao wa majaribio wa Moko.

"Nimetoa maelekezo kumpa Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi washirikiane na mwalimu kujua kama kila jambo limefuatwa. Lakini baada ya kujiridhisha ndio tujenge hoja Sh. milioni 117 zaidi wanazohitaji kuna sababu? Wamejiridhisha? Kama kuna shilingi yoyote imepotea my friend (rafiki yangu) lazima zirudi, hakuna mjadala, kama zimekwenda salama ziende salama tujenge hoja tutapataje, tutakuja, Mkurugenzi Sh. milioni 117 useme utatupa ngapi na serikali itatupa ngapi," alisema Mkuu huyo wa Mkoa.

Akasema inashangaza kuona Shule ya Sekondari ya Kwiro ambayo iko mjini, yenye walimu 28 na watumishi wasio walimu takribani 18, wanaolipwa mishahara na serikali, lakini bado shule imeendelea kushindwa kufanya vizuri ambapo katika shule 21 zenye A level, shule hiyo imeshika nafasi ya 13 licha ya kuwa mjini na serikali kuwekeza kwa kiwango kikubwa shuleni hapo.

Alisema wanahitaji Mkoa wa Morogoro kutoa angalau shule tatu kama sio nne kwenye kumi bora kitaifa, kwani maeneo mengine zipo shule ambazo ziko porini, mbali, zisizosaidika, zenye hali ngumu, lakini zimeendelea kufanya vizuri kitaifa.

"Shule ya kwanza kitaifa ni Kisimiri, iko porini kabisa, lakini inawashinda. Lazima tubadilike na lazima tujue shida ni nini. Ofisa elimu sekondari, lazima tubadilike, shule zote zenye kidato cha nne, kidato cha sita, kwanini hazifanyi vizuri," alisema na kuongeza:

"Lazima tuanzie mahali, vinginevyo mtatupa kazi ya kufanya, na kazi hiyo ni kuwaondoa kwenye nafasi zenu, kwasababu umeshindwa kusimamia... kwa hiyo mjomba ukajipange."

Kuhusu uhaba wa walimu, alisema Manispaa ya Morogoro ina walimu 692 wakiwamo ambao wana kipindi kimoja tu kwa wiki, ingawa wanapata mshahara, na kutaka walimu hao wote watolewe na kupelekwa kwenye halmashauri nyingine ambazo zina uhaba wa walimu.

## NBC yaongeza kiwango cha utoaji mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NBC imesema imeongeza ufanisi mkubwa katika utendaji wake ikiwamo kuongeza kiwango cha utoaji wa mikopo, huku ikitangaza kupata ongezeko la faida (baada ya kodi) la asilimia ya 367 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka huu, ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana.

Mafanikio hayo yanatajwa kusababishwa na ufanisi wa benki hiyo katika nyanja mbalimbali ikiwamo katika usimamizi wa mizania, kuongezeka kwa mapato yatokanayo na ada ya mihamala na kuboreshwa kwa huduma za mikopo, kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi.

Kwa mujibu wa ripoti yake ya kifedha ya robo tatu ya mwaka 2019 iliyotolewa hivi karibuni, hadi kufikia mwezi Septemba mwaka huu, benki hiyo ilikuwa na jumla mikopo yenye thamani ya Sh. 987 bilioni, huku ikiwa na amana za wateja zenye thamani ya Sh. trilioni 1.717.

"Jumla kuu ya mikopo yetu imeongezeka katika kipindi cha robo mwaka kwa asilimia 3.7, hasa ikichangiwa na ongezeko la uombaji wa mikopo kutoka kwa wateja wetu wakubwa, wa reja reja na wa kati, huku amana zetu kwa ujumla ziliongezeka kwa asilimia 19.3," aliongeza Sabi.

"Umakini na ufanisi wetu katika suala zima la utoaji wa mikopo limeanza kutupa faida kwa kuwa hata kiwango cha mikopo chechefu kimeendelea kupungua hadi kufikia asilimia 6.9 kutoka asilimia 10.1 katika kipindi kama hiki mwaka uliopita," alibainisha Sabi.

Aliongeza kuwa mkakati wa mabadiliko ya kidigitali unaotekelezwa na benki hiyo umeendelea kuzaa matunda ya ukuaji huo, huku akibainisha kuwa mfumo wa miamala kwa njia ya simu umekua kwa asilimia 50 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka jana.

"Ongezeko hili ni ishara kwamba wateja wetu wanapokea vizuri mabadiliko ya uboreshaji wa huduma zetu hasa kidigitali na hivyo kutupunguzia kiasi cha muda ambao tungeutumia kuwahudumia kupitia matawi yetu na hivyo tunajikuta tunapata muda wa kutosha kubuni na kutekeleza huduma nyingine bora zaidi kwa ajili yao," alisema.

Aidha, Sabi aliitaja huduma nyingine ya kielektroniki inayokua kwa kasi kuwa ni NBC Wakala ambayo kwa sasa ina mtandao wa mawakala zaidi ya 2,000 waliotapakaa nchi nzima.

"Wateja sasa wana uwezo wa kuzifikia akaunti zao na hufanya mihamala kwa urahisi zaidi kupitia maelfu haya ya mawakala nchi nzima."

# Mhandisi atumbuliwa tuhuma kusababisha hasara ya bil. 2/-

**Na Frank Monyo**

NAIBU Waziri wa Maji, Juma Aweso, amemsimamisha kazi Mhandisi Leonard Baseki, kwa kuihujumu serikali na kuisababishia hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 2 na kushindwa kukamilisha miradi ya maji ya Bungu, Mwanambaya, Mkerezange wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

Aweso, amechukua hatua hiyo baada ya kupata taarifa za miradi ya maji akiwa ziarani wilayani humo na kubaini utekelezaji mbovu, kutoridhishwa na utekelezaji wa miradi na ukiukwaji wa taratibu za kimkataba ambapo amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, kufuatilia suala hilo na kumsimamisha kazi mara moja mhandisi huyo kwa kuihujumu serikali.

Hatua hiyo ilichukuliwa mwishoni mwa wiki wakati Aweso akiwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya maji ikiwamo ya visima wilayani humo. Aweso akiwa ameongozana na viongozi mbalimbali wakiwamo kutoka Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa) na Ofisa wa Maji Bonde la Wami Ruvu, Simon Ngonyani, alisema mhandisi Baseka ameisababishia serikali hasara zaidi ya Sh. bilioni 2 na kushindwa kutekelezwa miradi hiyo kwa wakati huku akijenga tangi la maji bila kuwapo chanzo cha maji cha uhakika katika mradi wa Mwanambaya.

"Hii haiwezekani, mhandisi tena wa serikali anaharibu hapa Mkuranga halafu anahamishiwa sehemu nyingine na kule anaenda kuharibu pia, kwa hiyo nimemwagiza Katibu Mkuu (Profesa Mkumbo) amsimamishe kazi na apelekwe kwenye Bodi ya Wahandisi," alisema Aweso.

Aliongeza kuwa mpaka sasa wahandisi 95 wameshaondolewa kutokana na kutokukamilisha miradi kwa wakati na kuiingiza serikali hasara na kuchelewesha azma ya serikali ya kumtua mama ndoo kichwani.

"Nawaonya wahandisi wengine kuwa hatutafumbia macho pindi wanapohujumu serikali, tutawachukulia hatua ikiwamo kuwapeleka mbele ya kamati ya maadili," alisema.

Akizungumzia mradi wa maji wa Mkuranga unaosimamiwa na Dawasa, alimtaka mkandarasi wa mradi huo kwenda kwa haraka ili wananchi wapate maji kwa wakati kama makubaliano yalivyo kwenye mkataba.

Aweso, aliutaka Dawasa kufanya kikao cha pamoja na uongozi wa Halmashauri ya Mkuranga na kufanya usanifu wa mradi wa maji ili wakazi wote wa Mkuranga wapate maji kwa wakati ili kuondokana na shida waliyonayo.

"Nawapongeza Dawasa kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuendesha miradi, kwa fedha zao za ndani hili ni jambo kubwa sana tumeona Dar es Salaam wamefanya kazi nzuri na sasa wameamua kuja Mkuranga ili wananchi mpate majisafi na salama," alisema Aweso.


Distributed via ippmedia

Wafanya usafi wakiuondoa mchanga uliosababishwa na mvua kando ya Barabara ya Morogoro, eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wakulima wa tumbaku wakumbushwa mikataba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama imewataka wakulima wa tumbaku kuhakikisha wanalima tumbaku kulingana na mikataba waliongia na kampuni zinazonunua zao hilo.

Lengo la kuwakumbusha ni kupunguza malalamiko yanayojitokeza pindi tumbaku iliyozidi inaposhindwa kununuliwa.

Anamringi Macha ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, aliyabainisha hayo katika kikao cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri ya Msalala, na kusema wakulima wa tumbaku wamekuwa wakilima tumbaku nyingi kuliko makubaliano waliyoingia na kampuni.

Alisema msimu uliopita wakulima walitakiwa kulima kilo milioni saba kulingana na mikataba waliyoingia na kampuni, lakini walilima zaidi ya kilo mlioni 9.4, na kusababisha serikali kuingilia kati na kuwatafutia masoko.

"Madiwani tujitahidi kuwasisitiza wakulima kwenye kata zetu kulima tumbaku kulingana na mikataba waliyoingia na kampuni za tumbaku...hii itatusaidia kuondoa lawama za wakulima tumbaku itakapobaki na kukosa masoko," alisema Macha.

Pia, aliwataka wakulima wa zao hilo kuhakikisha wanalima mazao mbadala ya kibiashara kama mahindi, karanga, alizeti na mhogo ili kujiongezea kipato badala ya kuongeza uzalishaji kwenye tumbaku kinyume cha mikataba.

Katika hatua nyingine, Diwani wa Ikinda Matrida Musoma, alisema wakulima wa pamba wameuza pamba yao katika msimu uliopita, lakini mpaka sasa baadhi yao hajalipwa na kushindwa kujiandaa na msimu huu. Aidha, alisema kama wakulima watalipwa fedha zao kwa wakati, zitaweza kuwasaidia katika kununua pembejeo na kuwalipa vibarua kwa kuwa baadhi ya wakulima wako katika maandalizi ya kilimo hicho.

Naye Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Msalala, Zhedekia Solomon, alisema msimu wa kilimo cha pamba umeshaanza na kila mkulima atatakiwa kununua pembejeo na mbegu kwa fedha taslimu na sio mkopo.

Naye DC Macha aliomba kupata orodha ya wakulima wote wa pamba ambao mpaka sasa hawajalipwa ili kuweza kufuatilia malipo yao yamefikia katika hatua gani.

# Lema awashukia Wachina mradi wa maji wa bil. 520/-

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MBUNGE wa Arusha Mjini, Godbless Lema, amewalalamikia Wachina wanaopitisha mabomba ya mradi wa maji wa Sh. bilioni 520 unaotekelezwa Jiji la Arusha kwa kuharibu barabara bila kujali haki za binadamu.

Alitoa malalamiki hayo mwishoni mwa wiki kwenye Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Lema alisema mradi wa maji ni mzuri kwani utaondoa changamoto ya ukosefu wa maji katika jiji hilo ila vema ukatekelezwa kwa kujali haki za binadamu.

"Hawa wenzetu Wachina wanatekeleza mradi huu bila kujali haki zetu wananchi mfano sehemu ya kuchimba na kufikia kwa siku moja wanafukia baada ya siku tatu au zaidi," alisema.

Aidha, alisema hawajali na wameharibu barabara na kusababisha maeneo mengine kutopitika wakati wa mvua.

Lema alishauri vema Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (AUWSA) ikawasimamia Wachina hao ili wasiwafungie wananchi kwenye barabara zao na mageti ya kutokea kwenye nyumba za wananchi kutokana na kuchimba mitaro na kuacha wazi bila kufukia kwa zaidi ya siku tatu.

Alisema siku moja walipokuwa eneo la nyumba yake, alihakikisha hatoki eneo hilo kwa kuwasimamia ili wafukie mtaro wao.Naye Ofisa Uhusiano wa AUWSA, Willium Shayo, alisema suala hilo watasimamia, na kwamba kwa sasa wanakimbizana kuwaletea maji wananchi ndani ya mwezi huu.

Alisema wamechimba visima 11 eneo la Magereza ambavyo vitatoa maji lita milioni 24 kwa siku, na wanatarajia kazi ya kuingiza maji hayo kwenye mtandao wao itakamilika mwezi huu.



Mchuuzi wa matunda akilimenya nanasi kwa ajili ya kuwahudumia wateja wake, katika soko la Kilombero, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wenye sifa wakumbushwa kupiga kura uchaguzi mitaa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha, imewakumbusha wananchi wenye sifa ya kupiga kura kujitokeza kupiga kura kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba 24, mwaka huu.

Wito huo ulitolewa juzi na msimamizi wa uchaguzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Msena Bina, ambaye alisema muhimu kwa kila mwananchi kuhakikisha anatumia fursa hiyo kuchagua viongozi.

"Nawaomba sana mjitokeze kupigia kura na mpeane taarifa kwa wale wasiofahamu ili kufanikisha zoezi hili muhimu kwa afya ya taifa letu," alisema.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Arusha ina jumla ya kata 25 na ina vituo 155 na wenye sifa hizo ni wananchi wote raia wa Tanzania na wawe na umri wa miaka 18 na kuendelea pia wawe wakazi wa mtaa husika.

Bina alizitaja kata na idadi ya vituo vya kupigia kura kuwa ni Baraa vituo 8, Kimandolu 5, Levolos 2 , Moivaro 6, Moshono vituo 9, Olerien vituo 6, Ngarenaro vituo 5, Daraja Mbili vituo 6, Kaloleni vituo 3, Mjini Kati vituo 2, Themi vituo 5, Sekei vituo 7, Ungalimited vituo 6.

Zingine ni Elerai vituo 13, Engutoto vituo 6, Lemara vituo 7, Muriet vituo 13, Olasti vituo 5, Olmot vituo 6, Osunyai vituo 4, Sakina vituo 7, Sinoni vituo 7, Sokon One vituo 6, Sombetini vituo 4 na Terrat vituo 8.

# Chadema yalilia rafu wagombea

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Mkoa wa Arusha, kimelalamikia wagombea wake katika uchaguzi wa serikali za mtaa, kuporwa fomu za kugombea, kutekwa huku baadhi ya maeneo watendaji wa kata kufunga ofisi, wagombea hao wa upinzani wanaporejesha fomu za kugombea.

Aidha, chama hicho katika majimbo la Longido, Namanga na Loliondo kimedai watendaji wa kata hizo tangu juzi wamafunga ofisi, huku baadhi ya wagombea wake wakinyang'anywa fomu na watu wasiojulikana ambao huwa wamejificha katika ofisi hizo, kuvizia wagombea wa upinzani wanapokuwa wakirejesha.

Akiongea na vyombo vya habari katika kikao cha wagombea mbalimbali wa serikali za mtaa, Jimbo la Arusha Mjini, Katibu wa Chadema Mkoa wa Arusha, Elisa Mungule, alidai kuwa chama hicho kinahujumiwa ili wagombea wao wakose sifa za kushiriki uchaguzi huo kutokana na hofu walionayo Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Baada ya kutoa fomu kwa wagombea wa Chadema ofisi zote za kata zilifungwa hadi leo (juzi) ili wagombea wetu washindwe kuzirejesha, huku wagombea wa CCM wakipelekewa fomu nyumbani…hii si demokrasia hata kidogo," alidai Mungure.

Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, ameiambia serikali kupitia wingi wa wabunge wa CCM kutoa mapendekezo ya kufuta mfumo wa vyama vingi ili kibaki chama kimoja cha CCM, kuliko manyanyaso wanayofanyiwa wapinzani.

Lema alitoa kauli hiyo baada ya kutoridhishwa na mwenendo wa mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa kufuatia vitendo vya utekaji dhidi ya wagombea wa Chadema, huku wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi wakidaiwa kushiriki hujuma dhidi ya Chadema.

"Wagombea wetu wanatekwa kwa silaha, wanaporwa fomu za kugombea, wananyimwa fomu, wanapigwa na wanapoenda kulalamika Polisi wanaambiwa mnachezeana wenyewe kwa wenyewe," alisema Lema na kuongeza:

"Mimi ningekuwa na mamlaka ningewaambia wagombea waachane na uchaguzi huu," alisema Lema.

Baadhi ya wagombea wa mitaa, ambao wameeleza kunyanyaswa kwa kuchanwa kwa fomu zao wakati wakirejesha, kutekwa, kutishiwa maisha na kupigwa wamedai licha ya kupeleka malalamiko yao katika vituo kadhaa vya Polisi na kupatiwa hati ya mashtaka, lakini hakuna msaada wowote wanaopatiwa, hivyo kuhofia kupoteza sifa za kugombea nafasi hizo.

Baadhi ya wagombea hao waliokumbwa na kadhia hiyo ni Clotilda Aloyce ambaye ni mgombea wa Mtaa wa Olmuriaki Kata ya Sombetini, ambaye alidai wakiwa katika ofisi ya ofisa mtendaji walivamiwa na watu wasiojulikana wakawashambuliwa kwa kipigo na kuwataka wawapatie fomu.

Naye Renatus Kimario mgombea wa Mtaa wa Kijenge Kaskazini Kata ya Kimandolu, alidai kuwa juzi wakiwa wanahakiki fomu majira ya saa saba mchana, walivamiwa na watu watatu wakiwa na gari nyeupe ambao waliwatishia kwa bastola na kuwataka wawapatie fomu na baada ya kuzichukua waliondoka kwa kasi.

Naye Katibu wa Chadema Wilaya ya Arusha, Innocent Kisanyage, ameitaja mitaa katika Jiji la Arusha ambayo wagombea wake wamekumbwa na kadhia hiyo ni mtaa wa Sokoni One, Muriet, Olmoriaki na Longdong na kulitaka Jeshi la Polisi kutotumiwa na wanasiasa ili kuepuka kuvuruga katika uchaguzi huo.

Akizungumzia kadhia hizo, msimamizi wa uchaguzi katika Jimbo la Arusha Mjini, Msena Binna, amekiri kupokea malalamiko juu ya watendaji, kutoonekana kwenye ofisi zao na kudai kuwa suala hilo wamelishughulikia kikamilifu.

"Kwa upande wangu sina taarifa za mgombea kutekwa ila kama kuna mtu ametekwa anapaswa kutoa malalamiko Polisi kwa sababu ni kosa la jinai," alisema Binna.

Alisema malalamiko hayo ameyashughulikia kwa kiwango kikubwa na kama kuna mgombea amepata shida ampigie simu ili ashughulikie.

# Serikali yaonya uvuvi Nyumba ya Mungu

**Na Paul William,** MWANGA

SERIKALI imewataka wananchi wanaozunguka Bwawa la Nyumba ya Mungu, kuacha shughuli za uvuvi haramu, ikionya kuwa watakaokamatwa hawatatozwa faini, badala yake watafikishwa mahakamani ili wapewe adhabu ya kutumikia vifungo jela.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, Thomas Apson, wakati wa kuteketeza nyavu haramu na vyandarua 11, zote zikiwa na thamani ya Sh. milioni 75.3.

Apson alisema tatizo la uvuvi haramu katika eneo inalozunguka bwawa hilo limekuwa likishika kasi, akieleza kuwa anaamini kasi hiyo inachangiwa na utaratibu wa wavuvi wanapokamatwa, kutozwa faini kisha kuachiwa huru.

"Kwa sasa, serikali tumejipanga kuhakikisha tunakomesha biashara hii ya uvuvi haramu ambapo njia pekee tutakayokuwa tukiitumia kwa sasa tunapowakamata, hatutawatoza tena faini, bali tutawafikisha mahakamani ili mkahukumiwe kutumikia kifungo jela," alisema.

Kiongozi huyo wa serikali alisema wananchi ambao wamekuwa wakifanya uvuvi haramu, pia wamekuwa wakilitisha Jeshi la Polisi linapotekeleza majukumu yake kwa kuzuia biashara hiyo na kwamba hadi sasa, watu 14 wanashikiliwa kwa kutisha askari polisi.

Alisema endapo wananchi watafanya uvuvi kwa kufuata sheria, serikali itawasaidia kupata soko la uhakika la samaki ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuinua maendeleo yao.

Alisema bwawa hilo ni la thamani, lakini limekuwa likitumika vibaya kwa shughuli haramu.

Alisema kwa sasa, serikali inasaka wawekezaji watakaojenga hoteli za kitalii katika eneo la bwawa hilo ili litumike kwa shughuli za utalii. Ofisa Tarafa ya Lembeni, Gikila Maduhu, alisema nyavu hizo haramu zilikamatwa baada ya kufanyika kwa msako wa kushtukiza wa nyumba kwa nyumba katika vijiji vinavyozunguka bwawa hilo.

Maduhu aliiomba Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mwanga kuwasaidia kupata boti itakayokuwa ikitumika kwa kudhibiti uvuvi haramu katika bwawa hilo.



Diwani wa Kata ya Gararagua, Zakaria Lukumay (katikati), akitoa maelezo kwa Mbunge wa Siha, Dk. Godwin Mollel (kulia), kuhusu ujenzi wa choo cha kisasa katika Shule ya Msingi Magadini, wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro juzi. Mollel alihitimu elimu ya msingi shuleni hapo mwaka 1993. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# 'Jitokezeni mikutano ya kampeni uchaguzi mitaa'

**Na Paul William,** MOSHI

MJUMBE wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia vijana Mkoa wa Kilimanjaro, Wakili Zacharia Katikilo, amewataka wananchi kujitokeza katika mikutano ya kampeni ili kusikiliza sera za viongozi watakaowachagua kuongoza serikali za mitaa.

Wakili Katikilo alitoa rai hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, akieleza kuwa sasa ni wakati mwafaka wananchi kusikiliza sera na vipaumbele vya wagombea.

Wakili Katikilo alisema kwa kufanya hivyo, kutawarahisishia kuchagua kiongozi bora wanayemtaka kwa ajili ya kuwatumikia na kuwaletea maendeleo.

Alisema wapo baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakiwatumia vijana kufanya fujo katika kipindi cha kampeni na kutumia nafasi hiyo kuwataka vijana kujiepusha na wanasiasa wa aina hiyo.

"Sisi vijana tumekuwa tukitumika vibaya hasa katika kipindi hiki cha kampeni kusababisha fujo, tunapaswa kujiuliza kwanza tunanufaika na nini kupitia fujo hizo na tujiepushe nao wanasiasa hao ambao wanataka kuliingiza taifa katika machafuko na kupoteza taswira ya amani yetu," alishauri.

Akizungumzia tatizo la rushwa, Wakili Katikilo aliwataka wananchi kujiepusha kuwachagua viongozi wanaotoa rushwa kwa kuwa viongozi wa namna hiyo hawawezi kuwaletea maendeleo.

Alitumia nafasi hiyo kuiomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kuweka nguvu zaidi katika kufuatilia wagombea wa aina hiyo.

Alisema wananchi pia wanapaswa kuisaidia taasisi hiyo kuwaumbua wagombea watakaotoa rushwa kwa kuwa ni jukumu la kila raia kupambana na rushwa nchini.

# Wazindua kampeni kupanda miti

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KIKUNDI cha Amani 9 Arisi Marangu cha wilayani Moshi, kimezindua kampeni maalum ya kupanda miti zaidi 12,000 katika maeneo mbalimbali zikiwamo taasisi za serikali, dini na maeneo ya wazi ili kurejesha uoto wa asili.

Katibu wa kikundi hicho, Hance Moshi, alisema kampeni hiyo inatarajia kuhifadhi mazingira katika maeneo tofauti ya wilaya hiyo ukiwamo Mlima Kilimanjaro ili kuendelea kulinda theluji yake.

"Katika hatua za awali za kampeni yetu, leo tumeotesha miti 780 katika Shule ya Sekondari Mieresini ili kuwahamasisha wanafunzi kuona umuhimu wa hifadhi ya mazingira na tunaamini juhudi hizi watazipeleka katika makazi wanayoishi na itakuwa tabia yao," alisema.

Alisema kampeni hiyo inayoendeshwa chini ya Shirika la Mazingira la Floresta Tanzania, itadumu kwa zaidi ya miaka 20 ili kurejesha uoto wa asili ulipotea kutokana na shughuli za kibadamu katika maeneo tofauti, vikiwamo vyanzo vya maji.

Akizungumzia kampeni hiyo, Mkuu wa Shule ya Sekondari Mieresini, Fidelis Barnabas, aliiomba serikali kutunga sheria ya kudumu ya kutunza mazingira ili kila mwananchi alazimike kuitii badala ya kila taasisi kuwa na utaratibu wake.

"Juhudi zinazofanywa na kikundi hiki ni za kuungwa mkono kwani zimeongeza chachu ya shule yetu katika jitihada ambazo tumeziendeleza kwa muda mrefu, tutajiwekea utaratibu kila mwanafunzi aoteshe mti na kuutunza hadi amalizapo shule," alisema.

Naye mwanachama wa kikundi hicho, Jackson Shao, aliomba viongozi wa serikali za mitaa kuhakikisha wanatoa elimu juu ya utunzaji wa mazingira na athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira ili kazi yao iwe endelevu.

Nipashe
Spotika




**REKODI 5 ZA RONALDO KITABU CHA GUINNESS WORLD RECORDS** UK. 16&17

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Tammy Abrahamhas amefunga mabao saba katika mechi sita za ugenini mwanzoni mwa msimu huu wa Ligi Kuu England - ni Kevin Phillips mwaka 1999-00 (Sunderland) na washambuliaji wawili wa Manchester City, Edin Dzeko msimu wa 2011-12 pamoja na Sergio Aguero msimu wa 2016-17 (wote mabao nane) pekee waliofunga mabao mengi zaidi yake katika mechi sita za ugenini za mwanzo wa msimu wa ligi.







# HAKUNA TUTA!...

Sadio Mane akionekana kuchezewa madhambi ndani ya 18 na beki wa kulia wa Aston Villa, Frederic Guilbert, lakini mshambuliaji huyo wa Liverpool hakuzawadiwa penalti wakati wakishinda kwa mabao 2-1 kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Villa Park juzi, Jumamosi. **HABARI UK. 30**

SOKA




# SABABU 3 KWA NINI OZIL MUHIMU KUANZA ARSENAL

**LONDON,** England

AKIWA mshindi wa zamani wa Kombe la Dunia na Galactico, Mesut Ozil ameona kila kitu kwenye soka.

Baadhi ya watu waliona kwamba, safari ya Mjerumani huyo kwenda pale kwenye dimba la Emirates kama ni kujimaliza, lakini yeye aliona ni nafasi nzuri kucheza chini ya kocha anayemheshimu zaidi, Arsène Wenger.

**Hata hivyo, nyakati zile zimeondoka na Ozil sasa amejikuta yupo chini ya mtu tofauti kabisa, Unai Emery.**

Tangu siku ya kwanza ilionekana wazi kwamba, kocha huyo Mhispania Ozil walikuwa hawaangaliani usoni, na sasa ni mwaka na nusu, mambo yanaonekana kuwa mabaya zaidi.

Licha ya kuwa fiti, Ozil, mmoja wa wachezaji wanaolipwa mshahara mkubwa zaidi Arsenal, amecheza mara tatu tu msimu huu.

Sio tu kwamba ameondolewa kwenye kikosi cha kwanza, Unai Emery hakumweka kabisa kwenye kikosi katika mechi saba.

Na sasa mashabiki wa klabu hiyo wanaona kwamba, huu ni wakati muafaka kwa Ozil kuwapo kwenye mipango ya Emery na hii ni kwa sababu ya kuisaidia klabu hiyo.

Makala haya inakuchambulia sababu tatu kwa nini Arsenal inamhitaji Mesut Ozil kwenye kikosi cha kwanza, twende sasa...

**3. KUKOSEKANA KWA UBUNIFU**

Tangu alipotua pale Emirates, Unai Emery timu yake imekuwa ikicheza bila ubunifu eneo la boksi. Mhispania huyo anataka timu icheza kwa kujiachia uwanjani, huku mabeki wa pembeni wakipanda na kushuka.

Sasa mfumo huo umemfanya Ozil aonekana hana umuhimu pale katikati.

Msimu huu kwenye mechi za Ligi Kuu, Arsenal wamekuwa na wastani wa kutengeneza nafasi za kufunga 10.2 kwa mchezo. Ikilinganishwa na Manchester City wao wamekuwa na wastani wa 17.2.

Licha ya kucheza kwa dakika 71 kabla ya mwishoni mwa wiki dhidi ya Wolves, kwenye Ligi Kuu msimu huu Ozil bado ni mchezaji mbunifu zaidi. Wachezaji wenzake wamekuwa wakipata tabu sana bila yeye kuwa uwanjani na wamefunga mabao 13 msimu huu. Sababu pekee Arsenal wanapambana na kuwapo kwenye nne bora ni mabao ya Emerick-Aubameyang, ambaye pia amekuwa akiwalisha wenzake.

**2. USUMBUFU WA MASHABIKI**

Kila wakati kikosi cha Arsenal kikitangazwa kwenye mitandao ya kijamii, mashabiki wa Arsenal wanauliza, 'yuko wapi Ozil?' Ugomvi wa wachezaji na kocha sasa umeanza kuonekana dhahiri kwa mashabiki wa klabu hiyo.

Mashabiki wengi hawaangalii kipaji cha makinda Bukayo Saka na Joe Willock katika kikosi cha kwanza na kile wanachokifanya au kiwango cha Matteo Guendouzi msimu huu. Hata hamna shabiki mwenye muda wa kujadili kiwango bora cha Gabriel Martinelli kwenye michuano ya Ligi ya Europa.

Badala yake wote wanakuwa wakiuliza sababu ya kutochezeshwa kwa Ozil.

Arsenal wanamlipa Ozil zaidi ya pauni milioni moja kwa mwezi, lakini hapewi nafasi ya kucheza uwanjani.

**1. UMUHIMU WAKE KIKOSINI**

Wengi wanaweza kushutumu lugha ya mwili ya mchezaji huyo raia wa Ujerumani, lakini hakuna atakayekataa umuhimu wake ndani ya kikosi cha Arsenal. Tangu alipowasili England, 'Washika Bunduki' hao hawakufungwa kwa asilimia 80% ya mechi za ligi ambazo Ozil alikuwapo kikosini.

Katika mechi 167 alizocheza kwenye Ligi Kuu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amechangia mabao 84 ina maana kwamba bao moja katika kila mechi mbili.

Inawaumiza mashabiki namna Emery anavyoweza kutamka wazi kwamba hamhitaji mchezaji aina ya Ozil kwenye kikosi chake ambacho kimekuwa kikipata tabu sana kutafuta mabao.

Mara nyingi Mjerumani huyo amekuwa akitupiwa lawama wakati Washika Bunduki hao wanapofungwa katika mechi kubwa.

Alikuwa na pasi za mwisho 50 kwenye mechi 141 za Ligi Kuu, lakini sasa hafiti kwenye kikosi cha Emery.

Lakini yote kwa yote, Ozil bado ana umuhimu mkubwa zaidi kwa kikosi cha Arsenal na anahitajika zaidi kwa sasa kuliko wakati mwingine wowote.

**JE, WAJUA?**



LIVERPOOL imevuna pointi 31 kutokana na mechi 11 za Ligi Kuu msimu huu; katika historia ya ligi hiyo, ni Tottenham pekee msimu wa 1960-61 iliyovuna pointi nyingi zaidi (pointi 33) katika hatua kama hii ya michezo 11.

MICHEZO




KELVIN YONDANI

# REKODI ZA KUSHANGAZA LIGI KUU TANZANIA BARA

**Na Adam Fungamwango**

HIVI karibuni Tanzania imefanikiwa kuingia tena kwenye fainali za Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wanaocheza ndani ya nchi (CHAN).

**Ni baada ya kuiondoa Sudan kwa bao la ugenini, timu ya Tanzania, Taifa Stars ikifungwa bao 1-0 nyumbani, lakini ikipindua matokeo ugenini kwa kushinda mabao 2-1. Kwa matokeo hayo, Stars ikawa imefuzu fainali hizo kwa sababu imefunga mabao mengi ugenini.**

Mara ya kwanza, Stars ilifuzu michuano hiyo mwaka 2009 na kucheza fainali zake nchini Ivory Coast. Mwakani, michuano hiyo itafanyika nchini Cameroon.

Kwa sasa Watanzania wote wanaosubiria ni uteuzi wa wachezaji wa Taifa Stars ambao watakwenda kuiwakilisha nchi kwenye michuano hiyo ya CHAN.

Mwaka 2009, kulikuwa na kikosi cha wachezaji 23 kilichokwenda kuiwakilisha nchi kwenye michuano hiyo, ingawa hakikufanya vizuri sana kwenye fainali hizo.

Mwandishi wa makala haya anakusanya majina ya wachezaji waliokuwamo kwenye kikosi cha Stars kilichocheza fainali za CHAN nchini Ivory Coast mwaka 2009 ambao bado wanaendelea kucheza soka, hususan Ligi Kuu Tanzania Bara.

**1. ERASTO NYONI- BEKI**

Inawezekana kabisa akaweka rekodi ya kuwamo kwenye vikosi vyote viwili, cha mwaka 2009 na mwaka 2020.

Alikuwamo kwenye kikosi kilichocheza fainali ya CHAN nchini Ivory Coast na hadi leo amekuwamo kwenye vikosi vyote vya timu ya taifa iwe cha wachezaji wa ndani au mchanganyiko na wa nje.

Hadi leo amekuwa mchezaji tegemeo na ndiye aliyefunga bao la kwanza nchini Sudan, na kuchangia kuipeleka kwenye fainali hizo.

Wakati huo alikuwa akiichezea Azam FC, lakini kwa sasa bado yuko kwenye Ligi Kuu akiichezea Simba.

**2. KELVIN YONDANI - BEKI**

Ni beki mkakamavu ambaye pamoja na umri kuwa umekwenda, lakini bado ana uwezo wa hali ya juu kuwazidi mabeki vijana.

Si tu bado anacheza soka kwenye Ligi Kuu Tanzania akiwa na kikosi cha Yanga, lakini pia yumo kwenye timu ya Taifa, Taifa Stars iwe ya wachezaji na ndani au ya jumla.

Alikuwamo kwenye kikosi cha 2009 na nafasi yake inaonekana kabisa bado ipo kwenye kikosi kijacho. Alikuwa akiichezea Simba wakati akiwa kwenye kikosi cha CHAN 2009 lakini kwa sasa yupo Yanga.

**3. HENRY JOSEPH- KIUNGO**

Kiungo huyu alikuwapo kwenye kikosi cha CHAN mwaka 2009, wakati huo akiichezea Simba.

Hayuko kwenye kikosi cha Stars, lakini bado anaendelea kukipiga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa na kikosi cha Mtibwa Sugar.

**4. KIGI MAKASI- WINGA**

Kwa sasa anaichezea Ndanda FC kwa misimu kadhaa. Naye pia alikuwamo kwenye kikosi cha Stars kilichocheza fainali za CHAN 2009 nchini Ivory Coast.

Wakati anaitwa kwenye kikosi hicho alikuwa akikipiga kwenye klabu ya Yanga.

**5. MRISHO NGASSA- WINGA**

Anajulikana sana kama ni mchezaji mahiri kwenye kikosi cha Yanga. Huyu ndiye mchezaji aliyefanya makubwa na kuacha gumzo mchini Ivory Coast mwaka 2009.

Mpaka sasa bado Ngassa anaendelea kucheza soka la ushindani akiwa na klabu ya Yanga.

Itakumbukwa kuwa baada ya hapo alizunguka kwenye klabu mbalimbali ndani na nje ya nchi, zikiwamo timu za Azam, Simba, Mbeya City, Ndanda FC na hatimaye kurejea tena kwenye klabu ya Yanga.

**6. JERRY TEGETE- STRAIKA**

Ni straika ambaye mwaka 2009 akiwamo kwenye kikosi cha Stars kilichocheza CHAN wakati huo akiitwa akitokea kwenye Yanga.

Ni mmoja kati ya wachezaji wachache ambao bado wanaendelea kucheza Ligi Kuu, akiwa na kikosi cha Alliance ya Mwanza.

**7. NIZAR KHALFAN- KIUNGO**

Nizar ni mmoja kati ya viungo waliokuwa kwenye kiwango cha hali ya juu wakati huo hadi kuteuliwa kwenye kikosi cha CHAN akitokea kwenye klabu ya Moro United wakati huo.

Itakumbukwa kuwa kiungo huyo baadaye alizichezea klabu mbalimbali ikiwamo Yanga, Singida United na zinginezo. Kwa sasa bado anaendelea kucheza soka akiwa na klabu ya Pamba iliyo Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

**8. SHAABAN DIHILE- KIPA**

Kwa sasa ni kipa wa Green Warriors iliyo Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara. Kipa huyu wa zamani wa JKT Ruvu na Ruvu Shooting, alikuwamo kwenye kikosi cha CHAN mwaka 2009, wakati huo akiichezea JKT Ruvu.

**9. SHAABAN NDITI- BEKI**

Kwa sasa ndiye nahodha wa kikosi cha Mtibwa Sugar akiendelea kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara.

Nditi ni mmoja wa wachezaji waliounda kikosi cha CHAN kilichoiwakilisha Tanzania na bado anendelea kukipiga kama kawaida hadi leo hii. Hata wakati akiteuliwa alikuwa anatokea Mtibwa Sugar, ingawa alishawahi pia kuichezea Simba kwa muda mfupi.

**10. MWINYI KAZIMOTO- KIUNGO**


Mmoja wa wachezaji ambao bado hadi leo anacheza soka kwenye ngazi ya Ligi Kuu, tena kwa kiwango cha juu, ni Mwinyi Kazimoto.

Kwa sasa anaichezea JKT Tanzania kwa msimu wa pili sasa, akiwa ametokea kwenye klabu ya Simba.

Naye alikuwamo kwenye kikosi kilichoenda Ivory Coast kwenye michuano ya CHAN na hadi leo bado anakipiga kama kawaida. Alichaguliwa akiwa anaichezea JKT Ruvu ambayo ndiyo timu hiyo hiyo anayoichezea leo, tofauti ni kwamba imebadilishwa jina la kuitwa JKT Tanzania.

**NJE YA UWANJA**

AKIWA na umri wa miaka 21 na siku 26, Trent Alexander-Arnold juzi, Jumamosi aliichezea Liverpool mechi ya 100 kwenye mashindano yote. Tangu alipoanza kuichezea kwa mara ya kwanza Oktoba 2016, ni Roberto Firmino (36) na Mohamed Salah (28) wenye pasi nyingi za mwisho Liverpool kumshinda Alexander-Arnold (22).



# REKODI 5 ZA RONALDO KITABU CHA GUINNESS WORLD RECORDS



**TURIN,** Italia

KITABU cha Guinness World Records kiurahisi ni kitabu kinachotambulika kwa kuweka kumbukumbu za rekodi mbalimbali duniani. Tukiwa wakweli ni kwamba, kila mmoja wakati akiwa bado mdogo alikuwa na ndoto ya siku moja kuweka rekodi ambayo itaandikwa kwenye kitabu hicho.

**Kitabu hiki kinakupa heshima kubwa zaidi duniani kwa kuweka rekodi ambayo hakuna mtu mwingine ameifikia kwa nyanja mbalimbali.**

Lakini nyota wa Juventus, Cristiano Ronaldo, ambaye amejiwekea rekodi mbalimbali katika kile anachopenda kukifanya - mchezo wa soka umempa mafanikio makubwa zaidi.

Kwa zaidi ya miaka mingi, Ronaldo amejiwekea rekodi mbalimbali ambazo hakuna mchezaji mwingine wa soka amezifikia. Hapa tunaangalia rekodi tano ambazo Ronaldo ameziweka hadi sasa na zinatambulika na Kitabu cha Guinness World Records, shuka nazo sasa...

### 5. MWANAMICHEZO MWENYE WAFUASI WENGI ZAIDI FACEBOOK

Ronaldo amejiweka rekodi ya kuwa mmoja wa wanamichezo mwenye wafuasi wengi zaidi kwenye mtandao wa kijamii wa Facebook duniani.

Hadi sasa Ronaldo ana wafuasi 122,308,950 na kuwa mwanamichezo pekee duniani mwenye wafuasi hao.

Wakati wake akiwa pale Manchester United ndipo Ronaldo alipojijengea jina na kuwa mmoja wa watu maarufu zaidi.

Na mwaka 2009 anaweka rekodi ya kuwa mchezaji ghali zaidi duniani wakati alipohamia katika klabu ya Real Madrid, ambako alijiweka rekodi nyingi kwa kipindi chake chote cha uchezaji.

### 4. MTU MAARUFU MWENYE WAFUASI WENGI ZAIDI INSTAGRAM

Mtandano wa kijamii wa Instagram ni maarufu zaidi kwa watu maarufu duniani. Ni mtando unaotumika zaidi na watu maarufu duniani kwenye mtandao huo, ambao hutumiwa zaidi na wasanii na wanamichezo.

Wengine pengine walidhani kwamba, mtu maarufu kwenye mtandao huo angeweza kuwa mwanamuziki, lakini hali ni tofauti kwani, Ronaldo ana wafuasi 163,658,939.

Na pia Ronaldo tangu ametua Juventus ameongeza wafuasi wengi zaidi wa klabu hiyo kwenye mtandao wa kijamii. Kabla ya Ronaldo kutua hapo Juventus ilikuwa na wafuasi milioni 20, lakini baada ya kutua yeye wakaongeza haraka hadi milioni 31.18.

### 3. MCHEZAJI ALIYEFUNGA MFULULIZO LIGI YA MABINGWA ULAYA

Tena mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or amethibitisha kwamba, michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ni yake na imemfanya kuwa bora zaidi.

Ronaldo ndiye mfungaji bora wakati wote wa michuano hiyo, mchezaji aliyetoa pasi za mwisho nyingi zaidi, mfungaji wa 'hat-tricks' nyingi zaidi kwenye mashindano hayo.

Ronaldo msimu wa 2017-18 akiwa na Real Madrid alifunga katika mechi 11 mfululizo, akianzia msimu wa 2016-17.

### 2. MCHEZAJI ALIYEFUNGA MABAO MENGI LIGI YA MABINGWA ULAYA

Kitu kimoja kinachomtambulisha Ronaldo ni uwezo wake wa kuwa na kiwango mwendelezo, asiyechuja, kila msimu anakuwa na ubora zaidi.

Kuanzia msimu wa 2006-07 katika misimu 13, amefunga kwenye kila msimu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya zaidi ya mabao 20. Na hata kwenye timu ya taifa tangu alipoanza kuichezea mwaka 2004 hadi 2009 alifunga angalau bao moja kila mwaka.

Ronaldo ndiye mchezaji wa kwanza kufunga katika michuano minne tofauti ya Mataifa ya Ulaya, Euro. Alianza kuifungia nchi yake kwenye michuano ya Ulaya ya mwaka 2004 na akaendelea kufunga hadi ile ya mwaka 2016, ambapo Ureno ilitwaa taji lake la kwanza la kimataifa kwenye mashindano hayo.

Ronaldo pia ameingia kwenye rekodi sawa na gwiji wa Ufaransa, Michel Platin akiwa ameifungia nchi yake mabao tisa kwenye mashindano hayo.

### 1. AMEFUNGA MICHUANO MINNE YA KOMBE LA DUNIA

Kwenye mashindano ya Kombe la Dunia pia amejiwekea rekodi yake.

Ronaldo ameingia kwenye vitabu vya rekodi kwa kuwa mchezaji wa nne kufunga katika michuano minne tofauti ya Kombe la Dunia.

Licha ya kuwa hajawahi kulitwaa taji hilo, mwaka 2006 ambayo ndiyo ilikuwa michuano yake ya kwanza, walimaliza katika nafasi ya nne, nafasi bora zaidi kwa taifa la Ureno hadi sasa katika mashindano hayo.

Ronaldo alikuwa na kiwango bora zaidi kwenye mashindano ya Kombe la Dunia mwaka 2018, lakini licha ya mabao yake manne alishindwa kuivusha timu yake kwenye 16-bora.

Licha ya kwamba, hajawahi kuonja utamu wa kulibeba taji hilo, lakini rekodi yake inabaki kuwa bora zaidi kwa kufunga kwenye mashindano hayo manne tofauti.

## Nukuu


"Nini tena kinaweza kusemwa kuhusu yeye? Nimemaliza maneno, mara zote tunajua atatokea, kwa vyovyote mechi itakavyokuwa. Kipaji chake hakilinganishwi na kitu chochote; ukweli ni kwamba kila wakati anapogusa mpira, kitu cha kipekee hufanyika. Ana kipaji hicho ambacho hamna yeyote aliye nacho, siyo kwamba anaweza kucheza binafsi bali anafanya vitu ambavyo hakuna mtu anaviona, inatokea kwangu mara nyingine," **Kocha Mkuu wa Barcelona, Ernesto Valverde baada ya Lionel Messi kuonyesha kiwango cha juu wakati akiiwezesha timu hiyo kushinda mabao 5-1 dhidi ya Real Valladolid**



"Watu waliandika vitu kama: 'tutakuvunja miguu yako', 'tutamuua mke wako na ikiwezekana hata mtoto wako wa kike'. Hilo kwa kiasi kikubwa lilinitisha mimi na kuniacha kwenye wakati mgumu zaidi na hasira zikanifanya nifanye vile Jumapili," **nahodha wa Arsenal, Granit Xhaka akielezea sababu ya kukwaruzana na mashabiki wa timu hiyo kwenye mchezo dhidi ya Crystal Palace kwamba kulianzia katika mitandao.**



"Watu wengi walisema kwamba tunalishana kila mmoja [na Leo Messi], kwamba kuwa pamoja nchini Hispania kunatufanya bora. Hilo pengine ni kweli. Nilihisi uwapo wake zaidi nikiwa Madrid kuliko nikiwa Manchester. Ulikuwa ushindani mzuri. Tulikuwa nembo ya klabu. Awali ya yote, unahitaji kipaji, vinginevyo huwezi kuwa zaidi, hata hivyo, kipaji hakina maana bila kujituma zaidi, nisingeweza kuwa nilipo sasa pasipo utamaduni wa kujituma zaidi," **Cristiano Ronaldo.**





# REKODI ZA WACHEZAJI ZILIZONOGA LIGI KUU

AISHI MANULA

**Na Adam Fungamwango**

NI raundi ya 10 ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyokamilika mwishoni mwa wiki hii. Imeshaanza kuonyesha kuwa si ligi ya lelemama. Ni kwa sababu zinatafutwa timu mbili ama tatu kwa ajili ya kucheza mechi za kimataifa msimu ujao, huku pia zikitakiwa timu sita zishuke daraja.

**Ufafanuzi ni kwamba timu itakayoshika nafasi ya nne inaweza kucheza mechi ya kimataifa kama timu itakayoshika nafasi ya tatu mwishoni mwa ligi itatwaa Kombe la FA.**

Timu nne za mwisho zitashuka moja kwa moja, huku mbili zikicheza 'play off', nia ni msimu ujao kuwe na timu 18 badala ya 20 zilizopo sasa. Lengo ni kuwa na timu 16 tu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya misimu miwili ijao kwa matakwa ya waendeshaji wa ligi hiyo.

Wakati ligi inaendelea kushika kasi, wachezaji nao wamekuwa wakiweka rekodi mbalimbali na kuipendezesha Ligi Kuu Tanzania Bara. Mwandishi wa makala haya amekusanya rekodi mbalimbali tofauti zilizowekwa na wachezaji wanaocheza Ligi Kuu, hizi hapa...

### 1. MANULA ATIMIZA MECHI YA 100 KWA KICHAPO

Kipa wa Simba, Aishi Manula Jumatano iliyopita alitimiza mechi ya 100 akiwa na klabu ya Simba kwa kichapo kutoka kwa Mwadui FC.

Simba ilichapwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga ikiwa ni mechi ya kwanza kwenye Ligi Kuu tangu Mei 10, mwaka jana ilipopoteza dhidi ya Kagera Sugar kwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa rekodi zetu, Manula ametimiza idadi hiyo ya mechi akiwa na timu hiyo alipojiunga rasmi Agosti Mosi, 2017 akitokea Azam FC.

Idadi hiyo ni ya mechi zote za Ligi Kuu na michuano mbalimbali kama Kombe la Kagame, Mapinduzi Cup, Ligi ya Mabingwa, Kombe la Shirikisho na mengine.

Katika mechi hizo, ameondoka uwanjani bila kuruhusu bao kwa lugha ya wenzetu 'clean sheets' ni mechi 59, na mechi ambazo timu yake imeondoka na ushindi alipokaa golini ni 67. Mechi ambazo Manula alizokaa golini Simba ikiambulia vipigo ni 13, pamoja na ya Jumatano iliyopita, mechi 20 akikaa langoni timu yake ikitoka sare.

### 2. GERALD WA KWANZA KUIFUNGA SIMBA

Straika wa Mwadui FC, Gerald Mathias ndiye mchezaji wa kwanza kufunga bao msimu huu kwenye mechi ambayo Simba imepoteza.

Simba ilishinda mechi zote sita mfululizo msimu huu kabla ya kukutana na kipigo Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga.

Mara ya mwisho Simba kufungwa mabao na wachezaji wa timu pinzani huku ikipoteza mechi ilikuwa ni Aprili 20, mwaka huu, ikiwa ni Ligi Kuu msimu uliopita dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba. Wachezaji walioifunga Simba ikipoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Kagera Sugar ni Kassim Khamisi na Ramadhani Kapera.

Mara ya mwisho Simba kufungwa kwenye Ligi Kuu ilifungwa tena Mei 10, mwaka huu kwenye mechi ya mzunguko wa pili, Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar msimu uliopita, lakini lilikuwa ni bao la kujifunga wenyewe kupitia kwa Mohamed Hussein 'Tshabalala.'

### 3. DICKSON AFUNGA NA KUJIFUNGA MWENYEWE

Beki wa Mtibwa Sugar, Dickson Daudi ameingia kwenye vitabu vya kumbukumbu la soka Tanzania kwa kufunga bao na baadaye kujifunga mwenyewe kwenye mechi moja.

Rekodi hiyo ya mchezaji huyo kufunga mawili, moja likiwa la kujifunga aliiweka Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro Mtibwa ilipocheza dhidi ya Coastal Union na kushinda mabao 2-1.

Dickson alianza kuifungia Mtibwa dakika ya 20, lakini baadaye akajifunga dakika ya 49 na kuisawazishia Coastal. shukrani kwa bao la kujifunga la beki wa Coastal, Mtenje Juma ambalo ndilo lililoipa ushindi wa mabao 2-1 Mtibwa Sugar.

Mara ya mwisho kwa mchezaji kufunga mabao mawili kwenye mechi moja, moja akijifunga na lingine akiifungia timu yake ilikuwa ni Machi 5, 2016 kwenye mchezo kati ya Yanga dhidi ya Azam FC, Ligi Kuu msimu wa 2015/16. Iliwekwa na beki wa Yanga, Juma Abdul alipoifungia Yanga na kujifunga, timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2.

Tofauti yake ndogo ya Dickson ni kwamba Abdul yeye alianza kwa kujifunga dakika ya 10, kabla ya kusawazisha makosa yake kwa kuisawazishia timu yake dakika ya 28, kabla ya John Bocco wa Azam na Donald Ngoma wa Yanga wakati huo, kila mmoja kufunga bao na kufanya matokeo kuwa 2-2.

### 4. KYARUZI, IKOBELA WALIA KUIFUNGA MBEYA CITY

Wachezaji Erick Kyaruzi na Frank Ikobela wa Kagera Sugar walijikuta wakilengwa na machozi baada ya kuifunga timu yao ya zamani, Mbeya City.

Oktoba 24, kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, Kagera Sugar iliachia kipigo cha mabao 4-1, huku mauaji hayo yakiongozwa na Ikobela pamoja na Kyaruzi ambao msimu uliopita waliichezea Mbeya City na kujiwekea rekodi hiyo.

Kyaruzi alifunga bao la kwanza dakika ya 17 na Ikobela dakika 31 likiwa ni la tatu, lakini kila mmoja hakushangilia bao lake, badala yake walinyanyua mikono juu na kuomba msamaha kwa mashabiki wa Mbeya City, huku wakilengwa na machozi kwa kuifunga timu yao ya zamani.

### 5. LYANGA AFUNGA BAO LA KWANZA JKT TANZANIA

Straika za zamani wa Coastal Union, Simba, Singida United na Azam FC, Danny Lyanga amefunga bao lake la kwanza akiwa na timu yake mpya ya JKT Tanzania.

Ameweka rekodi hiyo akiifunga timu yake ya zamani ya Singida United Oktoba 30 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid mjini Arusha.

Katika mechi hiyo, JKT Tanzania iliichapa Singida United mabao 2-1. Lyanga alijiunga na timu hiyo akitokea Azam FC msimu uliopita alipomaliza ligi akiwa na mabao manne.

**NAJUA WAJUA**



MSHAMBULIAJI wa Wolves, Raul Jimenez amefunga mabao 11 katika mashindano yote msimu huu, ni Raheem Sterling na Sergio Aguero (13 kila mmoja) waliofunga mengi zaidi yake hadi sasa kwa wachezaji wa Ligi Kuu England.

SOKA



# KWA NINI NI MWAKA WA BARCA UEFA NA LALIGA

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA bado inaliwinda taji lake la sita la Ligi ya Mabingwa Ulaya na la kwanza chini ya kocha, Ernesto Valverde.

**Lionel Messi aliwaahidi mashabiki kabla ya kuanza kwa msimu wa 2018-19 kwamba timu itafanya kila linalowezekana kuweza kulibeba taji hilo na kulipeleka pale kwenye dimba la Camp Nou.**

Lakini wakajikuta wakiishia kwa Liverpool wakati walipofungwa kwenye nusu fainali ya mashindano hayo.

Nyota huyo wa Argentina alioonekana kama yupo kwenye uwezekano wa kulibeba taji hilo, lakini Barca ikaangukia pua kwa Liverpool.

Miamba hao wa Catalunya wamekuwa kwenye kiwango bora zaidi katika Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, ambapo wamelitwaa taji hilo mara nane katika miaka 11 iliyopita.

Lakini akili yao ipo zaidi kwenye kutaka kulibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na msimu huu Barcelona wanaonyesha ishara kwamba wanaweza kulibeba hilo mwishoni mwa msimu.

Sasa makala haya inakuchambulia sababu 3 kwa nini Barcelona wanaweza kulibeba taji la Ligi ya Mabingwa pamoja na lile la LaLiga msimu huu, shuka nayo...

### 3. KIKOSI KINA UWIANO BORA

Barcelona hatimaye wamepata uwiano mzuri zaidi kwa kikosi chao kwa sasa. Kwa kuwaongeza Antoine Griezmann, Frenkie de Jong, Junior Firpo, Ansu Fati na Carles Perez, Barca wameimarika katika kila idara.

Miamba hao wa Catalunya walikuwa na wakati mgumu msimu uliopita, kwani walikuwa hawana mbadala wa Jordi Alba, ambaye alionekana amechoka mwisho wa msimu. Lakini Ernesto Valverde amemtafutia msaidizi kwa kumleta beki wa kushoto wa Real Betis, Junior Firpo.

De Jong amekuwa anaimarisha safu ya kiungo ya Barca pamoja na Sergio Busquets na Arthur. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi amejiimarisha kwenye kikosi hicho kana kwamba alikuwa hapo kwa miongo mingi. De Jong amekuwa chaguo la kwanza kikosini hapo hata Ivan Rakitic amejikuta kwenye wakati mgumu wa kusaka namba kwenye kikosi cha kwanza.

Huku Griezmann pamoja na Fati na Perez wamepewa majukumu ya kuongoza mashambulizi mbele kwa Blaugrana hao, wakati Lionel Messi alikuwa majeruhi na Luis Suarez alikuwa akiimarisha mashambulizi kutoka kwenye winga. Sasa Messi amerudi dimbani, huku Suarez kiwango kikiwa kimepungua, Barca wana chaguo la kumtumia Ousmane Dembele kwenye winga ya kulia.

### 2. KUJIFUNZA KWA MAKOSA YALIYOPITA

Barcelona pengine ilikaribia kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya hivi karibuni, lakini wameshindwa kupambana hadi dakika ya mwisho. Miamba hao wa Hispania wameonyesha kutokuwa na kiwango mwendelezo kwenye mashindano hayo.

Wacatalunya hao walionekana kuishiwa nguvu wakiwa kwenye hatua muhimu kwenye msimu na ndio lilikuwa tatizo kubwa kwao. Sababu kubwa ilikuwa ni kukosekana kwa kikosi kipana.

Valverde amekuwa akitumia mfumo wa 4-3-3 na timu ilionekana kutokuwa na uzoefu nao. Hata hivyo, amekuwa akijifunza kutokana na makosa yaliyopita.

Valverde ameimarisha maeneo ambayo Barca yalionekana kuwasumbua msimu uliopita. Antoine Griezmann atakuwa mbadala wa muda mrefu wa Suarez, na tayari ameonyesha uimara wake pamoja na kiwango.

Frenkie de Jong amechukua nafasi ya Phillipe Coutinho, huku Nelson Semedo ameingia kwenye chaguo la kwanza pamoja na Sergi Roberto. Huku wachezaji vijana kama Fati na Perez wakionyesha ukomavu wao kwenye kikosi.

Pia timu imekuwa ikiimarika baada ya kupoteza pointi dhidi ya Granada na Athletic Bilbao mwanzoni mwa msimu wa ligi. Timu inaimarika na wachezaji wanazidi kuonyesha kujiamini.

### 1. KURUDI KWA KIWANGO CHA LIONEL MESSI

Lionel Messi alikuwa nje ya dimba kwa kipindi cha mwezi mmoja kabla ya msimu kuanza na lilikuwa pigo kubwa kwa miamba hao wa Catalunya. Raia huyo wa Argentina aliumia kigimbi na sasa anaonekana amepona na kuimarika vizuri kabisa.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, alikuwa kwenye wakati mgumu, lakini sasa anaonekana kurudi kwenye ubora wake.

Messi tayari ameonyesha kile ambacho Barca walikuwa wanakikosa na sasa ana mabao manne na pasi za mwisho tano kwenye mechi tano za LaLiga. Raia huyo wa Argentina alionyesha kiwango cha kuvutia dhidi ya Sevilla na Real Valladolid, na pia alifunga bao moja kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Slavia Praha.

Licha ya Barcelona kushindwa kwenye Ligi ya Mabingwa msimu uliopita, Messi alifunga mabao 12 na alikuwa mfungaji bora wa michuano hiyo. Pia alitwaa tuzo ya Kiatu cha Dhahabu msimu uliopita kwa kufunga mabao 36 kwenye LaLiga.

Ushindi kwa Barca ni muhimu pale tu Messi anapocheza katika kiwango chake. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, anapanga kuhakikisha analibeba taji hilo na kulipeleka pale Camp Nou.

TANGU Pierre-Emerick Aubameyang alipoanza kuichezea Arsenal kwa mara ya kwanza Februari 2018, yeye na Alexandre Lacazette kwa pamoja wamefunga mabao tisa kwenye Ligi Kuu England katika klabu hiyo, idadi ambayo ni kubwa zaidi kuwahi kufungwa kwa ushirikiano wa washambuliaji wawili katika historia ya klabu hiyo kwa kipindi kama hiki.



NDANI YA 18



KITABU cha Guinness World Records kiurahisi ni kitabu kinachotambulika kwa kuweka kumbukumbu za rekodi mbalimbali duniani. Tukiwa wakweli ni kwamba, kila mmoja wakati akiwa bado mdogo alikuwa na ndoto ya...

**Uk. 16&17**



# MAKOCHA WANAOWEZA KUMRITHI EMERY ARSENAL

**LONDON,** England

BAADA ya sare na Crystal Palace ambapo Arsenal walikuwa wanaongoza kwa mabao mawili, Unai Emery amejikuta kwenye presha kubwa.

**'Washika Bunduki' hao sasa wamejikuta nafasi ya tano (kabla ya mechi za juzi na jana) kwenye msimamo, wakipitwa pointi nne na Chelsea na Leicester na wakitofautiana pointi moja na Crystal Palace waliopo nafasi ya sita.**

Arsenal hadi sasa wana tofauti mbaya ya mabao katika timu tano za juu ikiwa na tofauti ya +1.

Wakati Chelsea inatofauti ya +8, Leicester +17, Liverpool +16 na Manchester City wana +25.

Kiukweli takwimu ya tofauti ya mabao ya Arsenal ni mbaya zaidi kuliko Manchester United, ambao wana +2 wakiwa nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi.

Sababu kubwa ya Arsenal kuwa na mwanzo mgumu msimu huu ni kutokana na kuwa na safu mbovu ya ulinzi. Wameruhusu kufungwa mabao 14 msimu huu.

Na sasa mashabiki wengi wa Arsenal wanaona kwamba tatizo kubwa ni kocha wao Unai Emery.

Huku kikosi hicho cha Emery kikiwa na utajiri wa vipaji vya washambuliaji kama Pierre-Emerick Aubameyang, Alexandre Lacazette, Nicolas Pepe na Gabriel Martinelli, kocha huyo amekuwa na tatizo kwenye ulinzi.

Wakati Emery akiwa hajathibitisha ubora wake, wengi wanaelewa kwamba, alikuwa na mafanikio makubwa pale Sevilla wakati akishinda mara tatu mfululizo taji la Ligi ya Europa.

Hata wakati wake akiwa kule PSG alikuwa na kiwango cha kuvutia. Emery alishinda taji la ligi mara moja katika misimu yake miwili pale Paris, na alikuwa kocha wa kwanza kuipa taji la Ligi Kuu PSG tangu msimu wa 2011-12.

Sasa baada ya kuonekana kutokuwa kwenye kiwango cha kuvuti pale Arsenal, mashabiki wengi wanaonekana wanahitaji kocha mpya, na makala haya yanakuchambulia makocha watatu wanaoweza kuchukua nafasi yake pale kwenye dimba la Emirates, twende pamoja...

**3. RAFA BENÍTEZ**

Huku Rafa Benitez kwa sasa akiwa nchini China, kurudi kwenye Ligi Kuu ya England kunaweza kumshawishi. Wakati akiwa pale Newcastle aliidhibiti timu kwa nidhamu na ufundi na alikuwa na safu imara ya ulinzi. Na hilo linamfanya kuwa na nafasi kubwa ya kupewa Arsenal.

Benitez ni kocha mwenye mbinu nyingi, mara kwa mara akibadilisha mfumo dhidi ya timu pinzani. Na hicho ndicho kitu wanachokihitaji Arsenal kwa sasa, kwani safu yao ya ulinzi imekuwa butu kabisa.

Raia huyo wa Hispania anapenda zaidi kutumia mfumo wa 4-2-3-1, huku akimuachia namba 10 ajiachie na pengine anaweza kumtumia zaidi Mesut Ozil.

Benitez ana uzoefu wa kutosha kwenye Ligi Kuu ya England akiwa amezinoa Liverpool, Chelsea na Newcastle.

**2. MASSIMILIANO ALLEGRI**

Massimiliano Allegri ni kocha mwenye mafanikio zaidi kwenye historia ya klabu ya Juventus. Allegri aliiongoza Juventus kushinda mataji matano mfululizo ya ligi pamoja na manne ya Italia na fainali mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Baada ya ujio wa Cristiano Ronaldo Allegri aliondoka na pia alionekana kuwa sababu ya kuondoka kwa wachezaji wakubwa kama Paul Pogba, Andrea Pirlo na Arturo Vidal.

Allegri alikuwa na mafanikio makubwa zaidi kwa kuimarisha safu ya ulinzi ya Juventus kwa kipindi chote alichokuwa hapo.

Juve kamwe haikuruhusu zaidi ya mabao 27 katika msimu mmoja wakati wa kipindi chake, na msimu bora zaidi ulikuwa ule wa 2015-16 wakati walipofungwa mabao 20 kwa msimu wote.

Allegri amekuwa akitumia mifumo tofauti, lakini mara nyingi alikuwa akitumia zaidi mfumo wa 4-3-3 na 4-2-3-1 na 3-5-2. Na mifumo hiyo ilikuwa ikimwezesha kuwa na safu imara ya ulinzi.

Allegri aliwahi kudokeza kwamba ana nia ya kufundisha Ligi Kuu ya England siku moja, na hivi karibuni alibainisha kwamba anajifunza lugha ya Kiingereza.

**1. JOSE MOURINHO**

Huyu ni mtu ambaye anapenda zaidi timu yake iwe na safu ngumu ya ulinzi. Jose Mourinho pengine anaweza kuwa mtu bora zaidi kwa kikosi cha Arsenal ili kuimarisha safu ya ulinzi.

Msimu wa Mourinho wa 2004-05 pale Chelsea bado unashikilia rekodi ya kufungwa mabao machache zaidi, akiwa amefungwa 15. Hadi mwisho wa msimu wake pale Chelsea, Mourinho hakumaliza akiwa chini ya tatu bora. Hata katika timu nyingine alizofundisha kama Porto, Chelsea, Inter Milan, Real Madrid, halafu Chelsea tena, alikuwa na rekodi nzuri ya safu bora ya ulinzi.

Uvumi kwamba, Mourinho anatajwa kuchukua mikoba ya Unai Emery pale Arsenal ni mzuri na unaweza kuisaidia timu hiyo.

Mourinho mara zote amekuwa muumini wa kutumia mfumo wa 4-3-2-1. Mfumo huo ulifanya kazi vizuri wakati akiwa pale Real Madrid, akiwa na Ozil kwenye namba 10. Kuunganika kwao tena kunaweza kuipa uimara zaidi Arsenal.

Mourinho kama akichukua mikoba ya kuinoa Arsenal, anaweza kuipa mafanikio, kwani ni mmoja wa makocha wenye hamasa kubwa kwa wachezaji wake.

**USILOLIJUA**



CHELSEA imeshinda mechi saba mfululizo za ugenini hadi sasa kwenye mashindano yote msimu huu, hivyo kufikia rekodi yao ya kushinda mechi nyingi ugenini katika historia ya klabu hiyo (kati ya Februari-Aprili 1989 ikiwa chini ya kocha Bobby Campbell ilishinda mechi saba za ugenini).





# Jiji lahitaji vyumba vya madarasa 109 sekondari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, inahitaji vyumba vya madarasa 109 katika shule za sekondari ili kuwezesha wanafunzi wote waliofaulu mitihani ya darasa la saba mwaka huu kuanza kidato cha kwanza mwezi Januari mwakani.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Meye wa Jiji hilo, Mchungaji David Mwashilindi, wakati wa kikao cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo alisema ujenzi wa vyumba hivyo unaendelea katika hatua mbalimbali.

Alisema lengo la halmashauri hiyo ni kuhakikisha watoto wote waliofaulu wanaanza masomo Januari bila kuwapo kwa kikwazo cha vyumba vya madarasa wala madawati.

Mwashilindi alisema miaka iliyopita baadhi ya watoto walikuwa wanachelewa kuanza masomo kutokana na maofisa elimu kutoandaa mapema matokeo ya watoto wa darasa la saba na kwamba mwaka huu waliandaa mapema. Alisema baada ya kupata idadi ya matokeo, halmashauri kwa kushirikiana na wananchi waliendelea na maandalizi na kwamba kwa tathmini iliyofanyika wana uhakika wa wanafunzi wote kuanza mapema.

"Miaka iliyopita wataalamu walikuwa wanashindwa kutushauri vizuri kulingana na matokeo ya wanafunzi, tulikuwa tunasubiri matokeo yatoke kwanza ndio tunaanza kukimbizana na vyumba, safari hii ni tofauti maana tulishauriwa mapema na tukaanza maandalizi mapema," alisema Mwashilindi.

Alisema wanapata ushirikiano mzuri kutoka kwa wananchi kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa na kwamba baadhi vimeshafikia hatua ya kuezekwa na vingine vipo kwenye hatua ya maboma.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji hilo, Oscar Kapinga, alisema wanafunzi waliofaulu wapo zaidi ya 9,200 na kwamba ufaulu umekuwa mzuri kutokana na ushirikiano mzuri kati ya walimu, halmashauri na wazazi.

Alisema ufaulu huo ni sawa na asilimia 92 ya lengo la halmashauri na kwamba wataendelea kusimamia sekta hiyo ili kuhakikisha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kinaongezeka na kuwa bora.Alisema halmashauri imetenga Sh. milioni 87 kwa ajili ya kushirikiana na wananchi kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa ambavyo vinatakiwa kwa ajili ya wanafunzi waliofaulu.

"Baraza limetuelekeza kuhakikisha watoto wote wanaanza masomo mwezi Januari shule zitakapokuwa zinafunguliwa, sasa kazi yetu ni kuhakikisha miundombinu inakuwa vizuri na ndio maana tupo kwenye maandalizi makubwa sana," alisema Kapinga.

Aidha, katika kuhakikisha Jiji hilo linakuwa miongoni mwa majiji bora duniani, Kapinga alisema jiji hilo limeanza kutekeleza miradi mingi ya maendeleo ambayo italing'arisha ikiwamo upimaji wa viwanja vipya vya makazi ambayo yatakuwa ya kisasa.



Mkazi wa Mji wa Mbalizi, mkoani Mbeya, akikokota baiskeli yake aliyoisheheni mikungu ya ndizi, akipeleka sokoni jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# CCM: Tutashinda zaidi ya 90% mitaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimesema kimejipanga kupata ushindi wa zaidi ya asilimia 90 kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu kwa madai kuwa kwa sasa kinakubalika kuliko chama chochote.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu wa chama hicho mkoa, Solomon Itunda, kwenye Kongamano la Jumuiya ya Vijana wa chama hicho (UVCC) lililopewa jina la 'kubwa kuliko'.

Alisema chama hicho kitapata ushindi kwenye maeneo mengi kutokana na kujipanga vizuri kuanzia mwanzo ikiwamo kuwahamasisha wanachama na wakereketwa wa chama hicho kujiandikisha na kuhamasishwa kujitokeza kupiga kura.

Vilevile, alisema chama hicho kilifanya vizuri kwenye mchakato wa kura za maoni za kuwapata wagombea kwa maelezo kuwa mchakato ulikuwa wa wazi na wa haki.

"Lakini pia maendeleo yaliyofanywa na serikali yetu ya awamu ya tano chini ya Rais na mwenyekiti wetu, Dk. John Magufuli yanatubeba, tumefanya vizuri kwenye sekta mbalimbali ikiwamo afya, elimu, miundombinu na huduma zingine za kijamii," alisema Itunda.

Itunda alisema chama hicho kimejipanga pia kupata ushindi mkubwa kwenye Uchaguzi Mkuu wa rais, wabunge na madiwani unaotarajiwa kufanyika mwakani, huku akimtaka Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' kutafuta kazi nyingine.

Alidai mbunge huyo pamoja na madiwani wa Chadema wasitarajie kushinda tena kwenye uchaguzi huo na badala yake kata zote pamoja na jimbo litarejea CCM.

# DC akerwa na mavazi ya kinamama yasiyo ya staha

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Wilaya ya Chunya, Mhandisi Maryprisca Mahundi, amekerwa na vitendo vya baadhi ya wanawake wilayani humo kuvaa mavazi yasiyokuwa na staha akidai ni kinyume cha maadili ya Kitanzania.

Aidha, alisema vitendo hivyo vinachochea ongezeko la maambukizi ya magonjwa ya zinaa vikiwamo Virusi vya Ukimwi kutokana na mavazi hayo kuchochea mapenzi. Kutokana na tatizo hilo, aliliagiza Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kutunga sheria ndogo ambazo zitakuwa zinatumika kudhibiti vitendo hivyo, huku akisisitiza kuwa wanawake hao wanawafundisha tabia mbaya watoto.

Mahundi alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo ambapo alisema vitendo hivyo vinazidi kuongezeka hasa nyakati za jioni.

Alisema baadhi ya wanawake wanavaa nguo fupi ambazo hazisitiri miili na wengine wanavaa nguo za kubana kisha kuanza kuzurura mtaani hali ambayo inaweza ikachochea pia ongezeko la vitendo vya ubakaji. "Ukipita mtaani jioni kuna baadhi ya wanawake wanatia aibu sana, lakini hatuna sheria za kuwabana, hivyo nawaomba madiwani mtusaidie kutunga sheria, vitendo hivyo vinawaharibu watoto wetu maana wanaiga na kuona ni kitu cha kawaida," alisema Mahundi.

Aidha, aliwataka madiwani kushirikiana na maofisa watendaji wa mitaa katika kuhamasisha ukusanyaji wa mapato ili kurahisisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika wilaya hiyo.

Vilevile, aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kujitokeza kwa wingi Novemba 24 kwenye vituo vya kupigia kura kwa ajili ya kuwachagua viongozi wa Serikali za Mitaa ambao watashirikiana na madiwani pamoja na watendaji kuwaletea maendeleo. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, alisema mwaka huu halmashauri hiyo inakusudia kukusanya Sh. bilioni 4.3.

Alisema kwa sasa hali ya ukusanyaji wa mapato ni nzuri kwa maelezo kuwa katika robo ya kwanza wameshafikia asilimia 25, na kwamba mpaka kufikia Julai mwakani watakuwa wamefikia asilimia 100.

Mwanginde alisema kwa sasa halmashauri yake imeandaa mikakati ya kuhakikisha inalifanya zao la korosho kuwa la kimkakati ili kuongeza pato la mwananchi mmoja mmoja na halmashauri kwa ujumla. Aliwataka wataalamu wa kilimo katika wilaya hiyo kuendelea kufanya tathmini na tafiti katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo ili kufanikisha azma hiyo.

Pia Mwanginde alitumia kikao hicho kuwatakia mtihani mwema wanafunzi wa kidato cha nne wanaotarajiwa kuanza kuifanya leo ambapo alisema wakifanya vizuri itakuwa heshima kwa wilaya.





# Wanaounda vikundi kudai fidia wapewa angalizo kali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewaagiza wananchi kuacha kuunda vikundi kwa ajili ya kupanga mikakati ya kudai fidia ya mali zitakazoathiriwa na ujenzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa, badala yake wawatumie viongozi wa serikali za mitaa ambao wanatambuliwa na serikali.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Isack Kamwelwe, alitoa onyo hilo wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko yenye urefu wa kilomita 112.3.

Kamwelwe alisema kumekuwa na tabia ya wananchi kuunda makundi ambayo yanakuja kuivuruga serikali kwa kudai fidia za watu walioathirika na miradi ya ujenzi kitu ambacho si sahihi, kinachotakiwa ni kuwatumia viongozi hao ili wafuatilie madai ya wananchi wa mitaa yao.

"Kumekuwa na tabia ya watu wachache kuunda kikundi cha kudai fidia pale wanapoona kuna mahali ujenzi unapita na kuathiri mali za watu, halafu watu hao huchangisha fedha wakidai fedha hizo hutumika kama nauli ya kuwafikisha sehemu husika wanayokwenda kufuatilia fidia, wananchi acheni tabia hiyo, tuwatumie viongozi wa ngazi ya mitaa," alisema Kamwelwe.

Alitolea mfano waathirika wa ujenzi wa uwanja wa Msalato ambapo kuna kamati iliundwa ya kufuatilia fidia, lakini cha kushangaza kamati hiyo Mwenyekiti wake anatokea Kigoma na Katibu anatokea wilaya ya Chemba, kitu ambacho hakileti uhalisia kwa sababu Msalato wao haiwahusu.

Alisema wale wanaounda vikundi kwa ajili ya kutaka kusaidia watu kudai fidia wajitokeze kugombea nafasi za uongozi wa serikali za mitaa ili waweze kuwasaidia wananchi na si kutumia vikundi wanavyoviunda.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, aliwataka wananchi kutumia fursa za miradi inayotekelezwa kwa ajili ya kujiinua kiuchumi katika maeneo mbalimbali.

Alisema miradi ya maendeleo inayotekelezwa itawasaidia kupanua wigo wa kuendeleza ujasiriamali wanao fanya katika maeneo mbalimbali.

Alisema lengo ni kuona wakazi wa Dodoma wanakuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanachangamkia fursa zilizopo ili kujiingizia kipato kupitia ujasiriamali ambao wanafanya katika maeneo mbalimbali.



Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mhandisi Isack Kamwelwe (katikati), akikagua mnara wa mawasiliano jamii, Wilaya ya Kondoa, mkoani Dodoma juzi. Mtandao huo wa intaneti unaotumia mawimbi ya televisheni umebuniwa na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM). **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## 88.6% wamiliki wa vyombo vya usafiri wanakiuka sheria

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imebaini asilimia 88.6 ya wamiliki wa vyombo vya usafirishaji hawatekelezi kikamilifu Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini namba sita ya mwaka 2004 kwa kutotoa mikataba ya ajira na likizo kwa madereva.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, wakati wa kikao cha mashauriano kati ya ofisi yake, na viongozi wa vyama vya wafanyakazi madereva na wamiliki hao nchini.

Mhagama alisema katika kushughulikia malalamiko kutoka kwa wafanyakazi wa sekta ya usafirishaji (madereva) ya kunyimwa haki zao za msingi na waajiri wao, serikali ilifanya ukaguzi maalumu uliolenga kubaini hali halisi ya utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini.

Alisema waajiri hawawapatii kabisa mikataba ya ajira na likizo ya mwaka kwa madereva wao, kuwafanyisha kazi kwa zaidi ya saa za kazi na kutowasajili katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

"Uchunguzi uliofanywa kati ya Julai 15 hadi Agosti 26, mwaka huu kwa kukagua kampuni au wamiliki wa vyombo vya usafirishaji 787 kutoka mikoa 24 tulibaini kati ya waliokaguliwa ni waajiri 90 pekee ndio wanatekeleza sheria ya kazi.

"Uchunguzi ulilenga kukagua kama madereva wanamikataba ya ajira, kukagua viwango vya mishahara kwa kulinganisha na agizo la serikali namba 196 kuhusu mishahara ya sekta binafsi la mwaka 2013.

"Pia tulikagua kama madereva wamesajiliwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii na kupokea malalamiko ya madereva kuhusu masuala ya saa za kazi na mambo mengine ya ajira," alisema.

Mhagama alisema ukaguzi huo umebaini kuwa hali ya utekelezaji wa sheria za kazi na kanuni zake katika sekta ya usafirishaji si ya kuridhisha, hali ambayo imechangiwa kwa kiasi kikubwa na uelewa mdogo kati ya waajiri na wafanyakazi na hivyo kusababisha kuwapo kwa malalamiko na migogoro ya mara kwa mara.

Kutokana na ukaguzi huo, Serikali na vyama vya wafanyakazi madereva na waajiri katika kikao kilichochukua takribani saa sita walifikia maazimio yaliyosainiwa na pande zote tayari kwa ajili ya utekelezaji.

Akisoma maazimo hayo, Waziri Mhagama alisema wameazimia mkataba wa ajira ulioboreshwa uanze kutumika na waajiri wote wawapatie madereva wao.

"Mwaka 2017, serikali ilitoa maagizo ya madereva kupewa mikataba ya ajira iliyoboreshwa, lakini utekelezaji wake haukuwa mzuri, kwa hiyo sasa ni lazima waajiri kutekeleza hili," alisema.

Mhagama alisema pia wameazimia, kanuni zinazoandaliwa na Wizara ya Uchukuzi zitengeneze mazingira yatakayoruhusu sheria za kazi kutekelezwa na waajiri.

Pia waliazimia kutolewa kwa elimu ya Sheria ya Kazi kwa vyama vya wamiliki wa vyombo vya usafirishaji na vyama vya madereva.

Alisema pia wameazimia kuwa ofisi ya kamishna wa kazi isimamie majadiliano ya pamoja baina ya vyama vya madereva na vyama vya wamiliki ili kufunga mikataba bora.

Alisema pia wameazimia waajiri waruhusu wafanyakazi kujiunga na vyama na kuanzisha matawi kwenye sehemu zao za kazi.

"Maazimio mengine ni kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo mimi nasimamia kuendelea kusimamia kikamilifu Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa weledi.

Mhagama alisema wameazimia vyama vya wafanyakazi na waajiri wapewe nakala ya taarifa ya ukaguzi uliofanyika Julai hadi Agosti, 2019 ili viweze kujadiliana na wanachama wao na kutoa mapendekezo ya namna ya kutatua changamoto.

Mhagama alisema kikao hicho kimeazimia kuendelea kuheshimu na kuthamini utu na heshima ya mtu kati ya madereva na waajiri.

Alisema pia wameazimia kufanyika kwa kikao kitakachojumuisha wizara zote zinazogusa sekta ya usafirishaji na madereva.

Naye Naibu Waziri, Kazi, Vijana na Ajira, Anthony Mavunde, alisema kufanyika kwa mafanikio kwa kikao hicho ni mwanzo mzuri wa kutatua changamoto katika sekta ya usafirishaji.

## Wenye ulemavu wapewa somo

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu, Stella Ikupa, amewataka watu wenye ulemavu kuchangamkia fursa za ujasiriamali zilizopo kwenye maeneo yao badala ya kujifungia majumbani huku wakitegemea kuomba omba.

Ikupa alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akifunga mafunzo ya wajasiriamali kwa makundi maalum ya watu wenye ulemavu yaliyofanyika kata ya Buigiri Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma.

Alisema serikali imetoa fursa mbalimbali za kujipatia kipato ikiwamo mafunzo ya ujasiriamali, hivyo hakuna sababu ya kujifungia ndani na kusubiri usaidiwe.

"Ulemavu usitumike kama kigezo cha kushindwa kujishughulisha na ujasiriamali wakati serikali imeshatoa fursa nyingi za kujikwamua kiuchumi," alisema.

Aliwataka wajasiriamali wanaokopeshwa mikopo kuhakikisha wanazitumia kwa malengo husika ya maendeleo ili waweze kukuza biashara zao.

"Fedha za mikopo siyo za ruzuku, bali zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa ikiwamo kukuza mitaji ya biashara zao, na urejeshwaji wa kwa wakati, ili watu wengine waweze kukopeshwa mikopo hiyo," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Nakua na Taifa Langu, Jessica Mshana, aliiomba serikali kuwaondolea changamoto zinazosababisha washindwe kufikia malengo yao.

Alisema kuwa walemavu hao wamejifunza kutengeneza bidhaa mbalimbali hivyo wanahitaji kutafutiwa masoko ya uhakika.

Naye Diwani wa Buigiri, Keneth Yindi, alisema watu hao wamepata mafunzo ya ufugaji ili kuwaondoa katika hali ya utegemezi badala ya kujisimamia wenyewe.





# Mke wa Rais afunguka ubora huduma za afya

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mwanamwema Shein, amesema kwa kuzingatia umuhimu wa wananchi kuwa na afya bora, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka kipaumbele katika sekta ya afya kwa kuimarisha huduma mbalimbali.

Alisema hayo wakati wa uzinduzi wa huduma za upimaji afya kwa wazee wanaoishi katika nyumba za wazee Sebleni na Welezo mjini Unguja.

Timu ya madaktari bingwa kutoka China, ilishirikiana na madaktari wazalendo waliendesha upimaji wa afya kwa wazee wanaoishi katika nyumba hizo, kutoa huduma za uchunguzi, dawa na ushauri.

Alisema ili kufanikisha dhamira hiyo, serikali imechukua hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu, kununua vifaa vya kisasa vya uchunguzi, kuongeza bajeti ya dawa, kuongeza madaktari na kusomesha vijana wake wa kada ya afya ndani na nje ya nchi.

Alisema kwa sasa, huduma za afya katika hospitali na vituo vya afya kote nchini zimeimarika na kutolewa bure kwa makundi maalum, ikiwa ni hatua ya kufanikisha malengo ya mwasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar, Hatati Abeid Amani Karume.

Alisema hatua ya washirika wa maendeleo, ikiwamo Jamhuri ya Watu wa China, kuunga mkono juhudi hizo kwa wataalamu wake kupima afya za wazee nchini, ni jambo la kutia moyo na linalopaswa kupongezwa.

Mwanamwema pia alitoa ombi maalum kwa Ubalozi wa China kutoa huduma za afya kwa wazee walioko katika kambi za wazee kisiwani Pemba. Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Asha Suleiman Idd, aliwashukuru madaktari hao kwa moyo wao wa kujitolea na kuona umuhimu wa kuwaenzi na kuwahudumia wazee wa Zanzibar. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Castico, alisema wazee wamekuwa wakikabiliwa na magonjwa mbalimbali, ikiwamo sukari, shinikizo la damu, kiharusi, macho, masikio na mengineyo, hivyo hatua ya Ubalozi wa China kutoa huduma za afya kwa kundi hilo ni ya kupongezwa.

Nyumba za wazee za Welezo na Sebleni zina jumla ya wazee 71, ambao serikali huwapatiwa huduma zote muhimu, zikiwamo za chakula, malazi, matibabu.



Madaktari Bingwa kutoka China, wakitoa huduma ya upimaji wa afya kwa wazee wa nyumba za wazee Sebleni na Welezo, Zanzibar, baada ya kuzinduliwa na mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mwanamwema Shein (hayupo pichani), Wilaya ya Mjini Unguja juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wahimizwa elimu ushindani kiteknolojia

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi mwaka huu, kuhakikisha wanaendelea na hatua inayofuata ya elimu ili wawe katika mazingira mazuri kuendana na maendeleo ya teknolojia.

Aliyasema hayo wakati wa mahafali ya darasa la sita na maandalizi katika shule ya maandalizi na msingi Herrhuter iliyoko Mwera. Alisema elimu ndiyo njia kuu na ya msingi katika kumkomboa mwanadamu katika maisha yake, hususani katika karne hii inayotegemea zaidi wasomi.

Alisema katika maisha ya sasa, maendeleo ya nchi yanategemea zaidi wasomi, hivyo wanafunzi wana jukumu kubwa kusoma kwa bidii ili kuendana na mfumo uliopo hivi sasa wa matumizi makubwa ya sayansi na teknolojia.

Waziri huyo pia aliwataka wazazi kuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na walimu na watoto wao ili kupata mafanikio katika masomo yao.

Alisema wapo baadhi ya wazazi hawatoi ushirikiano kwa walimu kwa kutohudhuria vikao mbalimbali vinavyoitishwa shuleni. Alisema Wizara ya Elimu Zanzibar, imeandaa utaratibu maalum wa kumpatia mtoto elimu iliyo bora, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuhakikisha watoto wote wanapata haki yao hiyo ya msingi.

Akisoma risala kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Mwajabu Abdallah Rashid, alisema mafanikio yaliyopatikana katika shule hiyo ni pamoja na kuongezeka idadi ya wanafunzi kila mwaka, kuwapo maktaba na kujengwa kwa madarasa mapya 10.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Owden Ndile, alipongeza serikali kupitia kwa wizara hiyo kwa kuendelea kuboresha sekta ya elimu na kuzipa nafasi shule binafsi kuendelea kufundisha watoto.

# Waziri ataja mbinu udhibiti wa saratani

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohamed, amewataka wananchi kutumia fursa za kupima afya zinazotolewa na serikali na asasi za kiraia za nje na ndani, ili kujikinga na maradhi mbalimbali ikiwamo saratani.

Alitoa rai hiyo wakati wa mkutano wa jumuiya zinazotoa huduma za upimaji na utoaji wa elimu kwa maradhi mbalimbali kwa wananchi nchini.

Alisema Zanzibar ni miongoni mwa nchi ambazo raia wake wanakumbwa na matatizo ya saratani ambayo yamekuwa yakisababisha vifo kwa kiasi kikubwa.

Alisema ni vyema wananchi wa Zanzibar wakatumia fursa hizo zinazotolewa na serikali, pale jumuiya za nje au za ndani zinapofanya upimaji wa afya katika maeneo yao ili kujua afya zao na hata kujikinga na maradhi.

Alisema serikali katika kuboresha huduma za afya, mara kwa mara imekuwa ikihakikisha upimaji wa afya unafanyika katika maeneo mbalimbali ya mijini na vijijini ili wananchi wa maeneo hayo wapate huduma hiyo muhimu.

Waziri huyo pia aliwataka wananchi kufanya mazoezi, kuzingatia lishe bora na kuwa na utamaduni wa kujua afya zao ikiwa ni hatua muhimu ya kujikinga na maradhi hayo.

Mwenyekiti wa jumuiya zinazojishughulisha na saratani, Dk. Marijani Msafiri, alisema saratani ya matiti ndiyo inaongoza kwa vifo kwa wanawake duniani.

Aliwataka wananchi kujenga utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara ili kujikinga na maradhi mbalimbali yasiyoambukiza ambayo yamekuwa tishio, ikiwamo saratani na shinikizo la damu.

Mkutano huo ulioshirikisha jumuiya mbalimbali za afya, ulianza kwa maandamano ya wauguzi, madaktari na vikundi vya mazoezi kuanzia kwenye Viwanja vya Maisara hadi Mnara wa Kumbukumbu Kisonge.

# Wakulima wa korosho Mtwara kupata neema msimu ununuzi

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

WAKATI wakulima wa korosho wakiendelea na msimu mpya wa korosho kwa mwaka 2019/20, wamehakikishiwa kuuwa wataendelea kuhudumiwa pamoja na kuhakikishiwa usalama wa fedha zao.

Wametangaziwa uhakika huo na Benki ya Taifa ya NBC, ambayo imesema itaendelea kuwahudumia na kuwahakikishia usalama wa fedha zao, huku ikisogeza huduma hizo karibu zaidi badala ya kusafiri umbali mrefu.

Akizungumza wakati wa Kongamano la Uwekezaji na Maonyesho ya Biashara mkoani Mtwara mwishoni mwa wiki, Meneja wa NBC Mkoa wa Mtwara, Job Nshatsi, alisema wameendelea kuwa mstari wa mbele kutuoa huduma za kibenki, ushauri na mafunzo ya kifedha na biashara yanayowezeha wateja wake ikiwamo wakulima na wafanyabiashara wa korosho.

Alisema katika kuhakikisha wakulima wananufaika na huduma zake wameendelea kuongeza mtandao wao wa mawakala katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha wakulima wanapata fedha kwa wakati, lakini pia kwa usalama kwa kuepuka kusafiri na fedha umbali na mrefu kwenda palipo na tawi la benki hiyo.

"NBC tunatoa huduma za kibenki maalumu kwa ajili ya kukuza na kuendeleza kilimo-biashara (agribusiness) kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi ya Kilimo nchini (PASS), tukiangalia sekta ya kilimo na mnyororo mzima wa thamani katika kilimo, na kwa Mtwara tutaendelea kutoa huduma ili kusaidia kukuza uzalishaji, uongezaji wa thamani na uuzaji wa zao la korosho," alisema Nshatsi.

Aidha, alisema benki hiyo kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), wanaendelea kutoa elimu za kifedha kwenye vikundi mbalimbali vya wajasiriamali lengo ikiwa ni kuwawezesha wajasiriamali hao kupata mbinu mbalimbali katika kuendesha biashara zao.

Baadhi ya wananchi waliohudhuria kongamano hilo waliziomba taasisi za kifedha kuendelea kuwapa elimu ya matumizi sahihi ya fedha hasa katika kipindi hiki cha msimu wa mavuno ya korosho.

"Tunapohudhuria makongamano tunatumaini tutapata elimu mbalimbali, lakini watu wa benki waendelee kutoa elimu ya matumizi sahihi ya fedha ili kuwa endelevu hasa kipindi hiki ambacho wakulima wanauza korosho wasaidiwe wajue baada ya kuuza fedha wanazozipata wanatakiwa kuziendeleza kwenye miradi mingine ya maendeleo," alisema Asha Chimae.

Naye mwanachi mwingine, Hansi Chilumba, alisema: "Wananchi wapo tayari kufanya kazi lakini kinachokosekana ni ujuzi na mtaji, ni vizuri benki kuendelea kutuwezesha hata mmoja mmoja ili kutimiza malengo kwa sababu kila mtu anakuwa na malengo yake, lakini tunapounda kikundi inakuwa ngumu kwa wote kukubali wazo la mmoja ili kulifanyia kazi.


Distributed via ippmedia

Meneja Masoko wa Benki ya DTB Tanzania, Sylvester Bahati (kushoto), akimkabidhi msimamizi mkuu wa kituo cha watoto yatima cha Dhi Nureyn, Faidh Said Abri, sehemu ya msaada wa magodoro zaidi ya 20, yaliyotolewa na benki hiyo, kwa ajili ya kituo hicho, kilichopo mkoani Iringa, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukatili kijinsia dhidi ya watoto waongezeka

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto vimeongezeka kutoka matukio 13,457 mwaka 2017 na kufikia 14,417 mwaka jana.

Aidha, imesema takwimu zinaonyesha vitendo vinavyoongoza ni vya ubakaji vikiwa na jumla ya matukio 5,557, mimba 2,692, kulawiti 1,157, shambulio 965 na kujeruhi matukio 705.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo wakati wa kongamano la vyombo vya habari kuhusu ajenda ya kitaifa ya wajibu wa wazazi na walezi katika malezi na matunzo ya familia.

Akisoma taarifa yake jana kwenye kongamano hilo, Mkurugenzi wa Idara Maendeleo ya Watoto, Mwajuma Magwiza, alisema mikoa inayoongoza kwa matukio ni Tanga, Mbeya, Mwanza, Arusha na Tabora.

Alisema kumekuwa na ongezeko la mmomonyoko wa maadili katika jamii na familia.

"Tumekuwa tukishuhudia watoto wakifanyiwa ukatili wa aina mbalimbali, huku wanaofanya vitendo hivyo kwa kiasi kikubwa wakiwa ni watu walio karibu na watoto, familia, ndugu, jamaa na marafiki. "Kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi za mwaka 2018, zinaonyesha vitendo vya ukatili kwa watoto vinaongezeka kutoka matukio 13,457 mwaka 2017 hadi matukio 14,419 mwaka 2018 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 6.6," alisema.

Alivitaja vitendo hivyo vya ukatili kuwa ni pamoja na ulawiti na ubakaji, mimba, ndoa za utotoni, vipigo na ukeketaji.

Alisema kulingana na utafiti uliofanywa na wizara kwa kushirikiana na wadau kwa kipindi cha mwezi Desemba 2017 hadi Januari 2018 katika Halmashauri 12 za Ilala, Kinondoni, Temeke, Kigamboni, Ubungo, Arusha, Iringa, Mbeya Jiji na Wilaya, Dodoma, Nyamagana na Ilemela ilibainika watoto 6,393 wanaoshi na kufanya kazi mitaani.

"Kati yao wasichana ni 1,528 na wavulana ni 4,865. Ilibainika watoto 1,385 kati ya hao waligundulika kufanya kazi za usiku mitaani, wasichana ni 410 na wavulana ni 975.

"Uwapo wa watoto hawa maeneo ya mitaani kwa kiasi kikubwa unatokana na kutowajibika kwa familia katika kumudu majukumu yao ya kutunza na kulea watoto."

Pia alisema taarifa ya utafiti wa afya ya mama na mtoto na viashiria vya malaria ya mwaka 2015/16 inaonyesha asilimia 25 ya kaya za mjini na asilimia 27 ya zile zilizopo vijijini zina watoto ambao hawaishi na wazazi wao japo mzazi mmoja au wote wapo hai.

Alisema takwimu za wizara ya mwaka huu zinaonyesha migogoro katika ndoa imeongezeka kutoka migogoro 13,382 mwaka 2018 hadi 16,832 kufikia mwezi Juni mwaka huu ikiwa ni sawa ongezeko la asilimia 26. Aidha, aliomba vyombo vya habari kusaidia ikiwa ni pamoja na kuanzisha vipindi maalum ili kuelimisha jamii.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mkurugenzi Msaidizi sehemu ya Malezi na Elimu ya Familia, Tausi Mwilima, alisema wizara imejipanga kuhakikisha elimu inawafikia wadau wote wakiwamo waandishi wa habari ambao mnapewa mafunzo.

## Bodaboda wataka elimu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA cha wamiliki na waendesha pikipiki mkoani Shinyanga (CHAWADAPI), wameiomba serikali kupatiwa elimu ya ujasiriamali na kukopeshwa mikopo ya riba nafuu ili wasitegemea waajiri wao wanapowanyang'anya pikipiki zao.

Ombi hilo lilitolewa na mwenyekiti wa chama hicho, Idisam Mapande, wakati wa kikao cha kutambulisha viongozi wapya wa mkoa kutoka Shinyanga, Kishapu na Kahama, na kusema vikundi vya waendesha daladala za pikipiki na bajaji wamesahaulika kupewa elimu ya ujasiriamali.

Alisema kuwa elimu ya ujasiriamali kwa waendesha daladala za pikipiki na bajaji imesahaulika na kuwapatia elimu hiyo vikundi vya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu, huku waendesha bodaboda wakiendelea kurandaranda mitaani wakati wanaponyang'anywa pikipiki na waajiri. Mapande alisema kama waendesha daladala watapatiwa elimu hiyo, itawawezesha kujitegemea na kununua pikipiki zao wenyewe na kutunza fedha na kutokuwa tegemezi kwenye jamii au kujiingiza kwenye vikundi vya uhalifu ambavyo asilimia kubwa wametoka huko.

"Tunaomba kupatiwa elimu ya usalama barabarani, uraia na ujasiriamali ili tuweze kuzitambua haki zetu na kuondokana na dhana ya kuwa tegemezi ama kujiingiza kwenye vikundi vya kihalifu wakati waajiri wetu wanapotunyang'anya pikipiki na bajaji," alisema Mapande.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa bajaji wilayani hapa, Hosea Kenisoni, alisema: "sisi kila siku tunadai haki, lakini sisi hatutekelezi wajibu, viongozi wa Jeshi la Polisi wanasema tusibebe mishkaki, lakini bado tunaendelea kubeba na kusababisha ajali kila siku."

Mwenyekiti wa Usalama Barabarani wilayani Kahama, Azani Saidi, alisema atahakikisha wanafanya makongamano ya ujasiriamali kwa waendesha daladala wote ili waweze kuwa na kazi mbadala na yenye tija.

Pia Saidi amemtaka Mkuu wa Kitengo cha Usalama wilayani hapa, Joseph Mgeli, kuhakikisha anawachukulia hatua za kisheria waendesha pikipiki wakaobainika kubeba abiria zaidi ya mmoja na asipomchukulia hatua, atawajikia mwenyewe kisheria.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Usalama Barabarani mkoani Shinyanga, Antony Gwandu, alisema hatasita kuwachukulia hatua za kisheria wendesha pikipiki na bajaji wote wanavunja sheria hasa kwa kupitia kwenye taa za barabarani bila kuruhusiwa.

HABARI KIMATAIFA

## UN wauongezea muda ujumbe wa amani

**DARFUR,** Sudan

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa limepiga kura ya kuviongezea muda wa mwaka mmoja zaidi vikosi vya pamoja vya usalama vya Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU) katika Jimbo la Magharibi mwa Sudan la Darfur.

Juhudi kubwa zinaendelea kufanywa na UN ili kuhakikisha amani endelevu na hali ya utulivu inapatikana katika Jimbo la Magharibi mwa Sudan la Darfur.

Azimio lililodhaminiwa na Uingereza pamoja na Ujerumani limemtaka Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres kuwasilisha ripoti na mapendekezo kwa baraza hilo, Januari, 31, ili kutathmini hali ilivyo Darfur.

Naibu Balozi wa Uingereza wa UN, Jonathan Allen, alisema ujumbe huo wa UN na AU ujulikanao kwa kifupi kama UNAMID unalo jukumu muhimu la kuweka mazingira mazuri ya amani na maridhiano hasa wakati huu wa mchakato wa amani.

Mwanadiplomasia huyo alisema kwa kuongeza muda kwa vikosi vya UNAMID, UN imetambua umuhimu wake katika kudumisha hali ya utulivu katika Jimbo la Darfur. Juni, mwaka huu, Baraza la Usalama la UN pia lilikubaliana kutoondoa ujumbe wa UNAMID hadi Oktoba 31. Baada ya hapo UN na AU walipendekeza kuuongezea muda ujumbe huo hadi Oktoba 31, 2020, uamuzi ambao umeshaidhinishwa.

Julai mwaka jana, Baraza hilo la Usalama pia lilipiga kura na kuamua kupunguza kwa idadi ya maofisa wa ujumbe wa UNAMID kufuatia hali ya utulivu kuanza kurudi na mizozo kupungua.

Lengo lilikuwa ni kuviondoa kabisa vikosi hivyo ifikapo Juni, 30 mwaka 2020. Mzozo wa Darfur ulianza mwaka 2003 baada ya raia weusi nchini humo kuanzisha uasi dhidi ya serikali baada ya kudai kuwa serikali ya Sudan ilikuwa inaongozwa kwa misingi ya ubaguzi wa rangi na ukabila.

Pia Serikali ya Khartoum ilidaiwa kuwapa silaha wanamgambo wa Kiarabu kuwashambulia raia weusi, madai ambayo serikali iliyakanusha. Mzozo wa Darfur uliendelea kwa muda wa miongo mitatu chini ya utawala wa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Omar al-Bashir wakati ambao Sudan ilishuhudia umwagikaji wa damu sio tu katika Jimbo la Darfur bali hata katika maeneo ya Blue Nile na Kordofan Kusini.

Utawala wa Al-Bashir uliangushwa Aprili mwaka huu, baada ya maandamano makubwa kushuhudiwa nchini humo kushinikiza mabadiliko katika uongozi na baada ya hapo makubaliano ya kugawana madaraka yalitiwa saini Agosti kati ya jeshi na waandamanaji ambao waliitaka serikali kufikia makubaliano ya amani na makundi yenye silaha katika muda wa miezi sita. **DW**

# Wanajeshi Mali wavamiwa kambini, 49 wauawa

**BAMAKO,** Mali

WANAMGAMBO wa Kaskazini Mashariki mwa Mali wamewaua wanajeshi 49 wa Mali katika shambulio lililotokea katika kambi kuu.

Mkuu wa Majeshi ya Mali aliandika katika ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Facebook.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa shambulio hilo linatajwa kuwa hatari zaidi na halijawahi kutokea katika kipindi cha miongo iliyopita.

Katika ukurasa wa mtandao wa kijamii wa Twitter, jeshi limeelezea kuwa shambulio hilo ni la kigaidi.

Mali imekuwa ikikabiliana na vurugu za mara kwa mara tangu mwaka 2012, wakati ambao wanamgambo wa Kiislamu waliposhambulia kaskazini mwa nchi hiyo.

**Kundi la Ansarul Islam, likimaanisha kuwa watetezi wa dini ya kiislamu, lilianzishwa mwaka 2016 na mhubiri maarufu Ibrahim Malam Dicko.**

Wakisaidiwa na Jeshi la Ufaransa, Jeshi la Mali lilikuwa linalinda usalama wa eneo hilo, lakini bado vurugu zinaendelea.

Vurugu hizo zimezidi kuenea hata katika mataifa mengine ya jirani.

Awali iliripotiwa kuwa askari 54 waliuawa, taarifa aliyoitoa Msemaji wa Serikali, Yaya Sangare.

Hadi jana, hakuna kikosi cha kigaidi ambacho kimekiri kuhusika na shambulio hilo katika maeneo ya Indelimane huko Menaka.

Askari 38 waliuawa wakati ambapo kambi mbili za jeshi zilipovamiwa karibu na mpaka wa Burkina Faso mwishoni mwa mwezi Septemba.

Mali pamoja na Burkina Faso, Chad, Niger na Mauritania, ni miongoni mwa nchi ambazo majeshi yao yanafadhiliwa na Ufaransa.

Hata hivyo, vikosi vitano vya taifa vinaeleza kuwa wajumbe wa Ansarul walishambulia katika shambulio la Septemba.

Kundi la Ansarul Islam, likimaanisha kuwa watetezi wa dini ya kiislamu, lilianzishwa mwaka 2016 na mhubiri maarufu Ibrahim Malam Dicko.

Mwaka 2012, iliripotiwa kuwa wanamgambo wa kiislamu Kaskazini mwa Mali walishambulia eneo hilo. **BBC**



Waandamanaji kutoka mji wa Hong Kong wakiwa mitaani wakidai uhuru kamili kutoka China. **PICHA: REUTERS**

# Waandamana mitaani kudai uhuru kamili

**HONG KONG,** China

MAELFU ya waandamanaji waliojifunika nyuso wamekiuka agizo la Jeshi la Polisi na kuingia katika mitaa mikuu ya maduka mjini Hong Kong, kuwalazimu polisi kutumia mabomu ya kutoa machozi kuwatawanya.

Maandamano mapya yalianza mjini humo wakati kukiwa na wasiwasi kwamba China inapanga kuzidisha udhibiti wake katika mji huo.

Kiasi cha waandamanaji 3,000 walikusanyika katika viwanja vya Victoria Park, eneo ambalo limekuwa kitovu cha maandamano. Hata hivyo, Polisi walitumia mabomu ya kutoa machozi kutawanya maandamano ambayo mamlaka zinasema hayakuwa na kibali cha kufanyika.

"Serikali nzima inadhibitiwa na serikali kuu hivi sasa, kwa hiyo tumekuja hapa kuandamana ili kulinda uhuru wetu tunaostahili," alisema kijana mmoja wa miaka 17 alipozungumza na AFP.

Mwishoni mwa wiki China ilitangaza kuwa haitovumilia upinzani wowote wa kuingilia mfumo wa serikali wa Hong Kong. Pia inapanga kuongeza elimu ya uzalendo mjini Hong Kong.

Baadhi ya waandamanaji walimiminika mitaani kwenye eneo la maduka la Causeway Bay. Polisi wa kupambana na ghasia walikuwapo eneo hilo na kufanya upekuzi huku wakionya kwamba mkusanyiko wowote si halali.

Hata hivyo waandamanaji wengi walikaidi marufuku ya serikali ya kuficha nyuso zao na vitambaa maalumu. Wengi walivaa vifaa maalum vya kujikinga mabomu ya kutoa machozi.

Mwanaharakati wa kudai demokrasia, Joshua Wong aliwahamasisha watu 100,000 kushiriki maandamano hayo ya kupinga serikali.

Aliandika kupitia mtandao wa kijamii wa Twitter kwamba: "Utekelezaji wa uhuru wa mkusanyiko umezidi kuwa mgumu kwa sababu Polisi wa Hong Kong wamekuwa wakitumia nguvu katika miezi ya hivi karibuni. Ndio! Hatukati tamaa juu ya haki yetu ya kikatiba".

Mwanaharakati huyo ameyaelezea maandamano mapya kama wito wa dharura wa ongezeko la kudai uhuru kamili.

Waandamanaji wengi walibeba bendera za Uingereza au zile za kikoloni kwa kuzingatia ahadi iliyotolewa na Uingereza mwaka 1997 wakati wa makabidhiano.

Maandamano ya Hong Kong yalianza Juni mwaka huu kupinga pendekezo la kuwaruhusu wahalifu kushtakiwa China. Katika miezi iliyofuata, waandamanaji walianza kudai uchaguzi wa moja kwa moja kwa ajili ya viongozi wa Hong Kong. **DW**

# Wahandisi wanawake wafundishwa kutengeneza umeme bila kuzimwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WAKATI serikali ikielekeza nguvu zake kukuza uchumi kupitia sekta ya viwanda kuboresha na kuimarisha vyanzo vya uhakika vya upatikanaji wa umeme ukiwemo mradi mkubwa wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji, wa Julius Nyerere utakaozalisha megawati 2115, jitihada hizo zimeendelea kuungwa mkono na wadau wengine kwa kuhakikisha umeme unaozalishwa haupotei njiani hivyo kuwa kero kwa watumiaji wakiwamo wawekezaji.

Mkakati huo wa kudhibiti upotevu wa umeme, umeanza kufanywa kwa kuanza kutolewa mafunzo kwa wahandisi wa umeme wanawake 40 kutoka maeneo mbalimbali nchini, walioanza kujifunza matengenezo ya umeme bila kuzima.

Lengo ni maeneo mengine wautumie kufanya kazi hizo, tofauti na sasa ambapo matengenezo yamekuwa yakifanyika kwa kuzima umeme na kusababisha hasara kubwa kwa watumiaji na Taifa kwa ujumla.

Donald Mwakamele, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Afrique Live Power Line Maintenance T and D Limited, waliojitolea kuwafundisha bure wahandisi hao wanawake, kwa kuamini kuwa watasaidia kusambaza teknolojia hiyo katika maeneo mengine, na kutumika kufanya matengenezo ya umeme bila kuzima kwa madai mwanamke akipewa nafasi ya kusimamia jambo lolote huwa makini na ni vigumu kuharibu.

Alibainisha kilichomsukuma kujitolea kufundisha teknolojia hiyo ngeni kwa hapa nchini, ni kuunga mkono jitihada za Rais John Magufuli, ambaye amekuwa akihakikisha viwanda vingi vipya vinaanzishwa, vinafufuliwa na kuwakaribisha wawekezaji wapya zaidi kuwekeza nchini, mambo ambayo hayawezi kufanikiwa kama kutakuwa hakuna uhakika wa umeme.

"Tanesco wenyewe hawataki kusikia umeme unazimwa, ndio maana nimeingia nao mkataba wa miaka mitano wa kufanya matengenezo na tutakaowatumia kwa kazi hii ni hawa hawa mainjinia ambao tumewapata kupitia Bodi ya Wahandisi wa Umeme, ERB, na watafundishwa teknolojia hii," alisema Mwakamele na kuongeza:

"Sasa watashiriki kuunga mkono jitihada za Rais kwa kuhakikisha umeme haukatiki na kuondoa malalamiko ya wawekezaji ya kukatika ovyo kwa umeme na kushusha uwekezaji."

Alisema umeme unaozalishwa kwa sasa na Tanesco ni wa ukubwa wa Kilo-votts (KV) 220, lakini wahandisi hao watafundishwa kutengeneza umeme mkubwa zaidi kufikia Kilo votts (KV) 400 kwani matarajio ya Serikali ni kuhakikisha Tanzania itazalisha umeme mkubwa zaidi kukidhi mahitaji ya watumiaji vikiwamo viwanda na watu binafsi.

Mkurugenzi huyo alisema wanakusudia kuingia makubaliano na Chuo cha Teknolojia cha (DIT), ili kuwapa mafunzo na kuwatambua wahandisi hao, sambamba na chuo cha Umeme cha nchini Zambia ambako amekuwa akishirikiana nao kwa kazi na mafunzo na kuahidi mafunzo hayo kwa wahandisi wanawake, yatatolewa baadaye kwa nchi za Afrika Mashariki, huku akihimiza Zanzibar nao kuwapeleka wahandisi wanawake kujifunza.

Kwa upande wao wahandisi hao wanawake, Lightness Salema, Dainess Uwezo na Milka Manyasi walishukuru kupata fursa hiyo waliyoitamani muda mrefu, kwani chuoni mara zote walifundishwa ukitaka kutengeneza umeme ni lazima uzime.



Ofisa Manunuzi wa Manispaa ya Ilala, Vincent Leonard (wa pili kulia), akigawa vipeperushi kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mbonea, wakati wa semina iliyoandaliwa na Shirika la Utekelezaji wa Haki za Jamii (AJISO), kuhusu elimu ya haki za binadamu shuleni hapo, eneo la Kitunda Kivule, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa shirika hilo, Virginia Silayo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Tigo yatangaza kuungana rasmi na Zantel

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Mawasiliano ya MIC Tanzania Public Limited Company (Tigo), imetangaza rasmi kuungana na kampuni ya Zanzibar Telecom Public Limited Company (Zantel), baada ya kukamilika kwa taratibu zote za kisheria na kiumiliki ambapo lengo kuu ni kukuza na kuboresha huduma za mawasiliano nchini.

Pamoja na kupata vibali kutoka mamlaka zinazohusika, mchakato wa kuhamisha hisa na umiliki kamili kutoka Zantel kwenda Tigo sasa umeshakamilika. Kufuatia kukamilika kwa zoezi hili sasa kampuni hizo zitaunganisha shughuli zake za kiutendaji Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar.

Akizungumza kuhusu muungano huo, Mkurugenzi Mkuu wa Tigo, Simon Karikari, alisema hatua hiyo ina manufaa makubwa kwa Taifa," alisema na kuongeza:

"Ninaamini kuwa kuunganishwa kwa kampuni hizi - Tigo na Zantel kutajenga huduma jumuishi kwa Watanzania wote siku za usoni. Wateja wote wa Tigo na Zantel wataweza kufurahia huduma bora kutoka kwenye soko imara litakalosaidia kuchochea ubunifu kwenye sekta ya mawasiliano."

Muunganiko wa kampuni hizi mbili utasaidia katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa wateja wa Tigo na Zantel waliopo kote Tanzania Bara na Visiwani.

Aidha, muungano huu utawezesha kupanua wigo wa huduma zetu pamoja na kuongeza ubora wa upatikanaji wa mawasiliano katika maeneo ya mijini na vijijini.

Vile vile muungano huu utasaidia katika usambazaji wa huduma za mawasiliano kwa kampuni na taasisi mbalimbali nchini na pia kupanua huduma za kifedha kwa njia ya simu za mkononi.

"Tunategemea mafanikio chanya kutokana na muunganiko wa kampuni hizi wenye lengo la kuchangia kwenye maendeleo ya Taifa," alisema na kuongeza:

"Zoezi la kuunganisha taratibu za kiutendaji wa kampuni hizi zinatazamiwa kuanza hivi punde. Aidha, wateja wa Tigo na Zantel wataendelea kupata huduma bila usumbufu wowote kutoka mtandao husika kwani namba na laini za wateja hazitabadilika."

# Bilioni 10/- kuleta fursa maji Ziwa Victoria

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

SERIKALI imeamua kupeleka maji katika Kata ya Kigwa wilayani Uyui mkoani Tabora kupitia mradi wa ujenzi wa bomba la maji kutoka Ziwa Victoria kwa gharama isiyopungua Sh. bilioni 10.

Fursa hiyo ilitangazwa jana na Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, baada ya kusikia kilio cha wakazi wa Kigwa cha maji akiwa katika ziara ya kusikiliza kero za wananchi.

Alisema kuwa eneo hilo hakuna mto wala bwawa na ndio maana katika kata hiyo kuna tatizo kubwa la maji na ndio maana serikali imesikia kilio chao na kuamua kutatua tatizo la wananchi hao.

Waziri huyo alisema kama serikali imeweza kutoa maji kutoka Ziwa Victoria, haiwezekani kushindwa kupeleka maji kwa wakazi wa Kigwa ambao wako umbali wa kilometa 29 kutoka bomba kuu.

Prof. Mbawara alisema ukikamilika utasaidia kuwanufaisha vijiji 16 vya Jimbo la Igalula.

Alisema utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza Desemba mwaka huu, na kuongeza kuwa utekelezaji wa ujenzi wake utawahusisha vijana wa Kigwa,

Mbunge wa Igalula, Mussa Ntimizi, aliishukuru serikali kwa uamuzi wake wa kuchukua maji kutoka mradi wa bomba la Ziwa Victoria na kuwapelekea baadhi ya wakazi wa jimbo hilo, ambalo lilikuwa limesahaulika katika mradi wa kwanza wa kuleta maji mkoani Tabora.

Alisema hatua hiyo na ile ya kutekeleza mradi wa Tura itasaidi kuwatua ndoo wanawake wa Kigwa kama walivyoahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015.

Naye Mkazi wa Kigwa, Dotto Mrisho, alisema kuwa 2010 walijengewa tangi la maji ambapo yalitoka siku alipofika Waziri Mkuu wakati ule, Mizengo Pinda, lakini baada ya kuondoka hakuna maji tena toka siku ile hadi sasa.

Alisema kitendo kile kiliwavunja moyo na kuona kila anapokuja kiongozi anapowaambia kuwa wataletewa maji wanajua kuwa wanadanganywa.

Mrisho alisema kuwa anaamini juhudi za serikali ya sasa itawasaidia kuwaondolea kero ya maji katika eneo lao la Kigwa.

Semeni Misana, alisema tatizo la maji katika eneo hilo ni kubwa jambo linalowafanya waamke usiku sana kutafuta maji ambapo wakati mwingine wanakabiliwa na matatizo mengi ikiwamo kukataliwa na wenye visima.



# VALVERDE AKATAA KUJIUZULU BARCELONA

**VALENCIA,** Hispania

ERNESTO Valverde alikataa kujibu swali kwamba endapo atajiuzulu kama kocha wa Barcelona baada ya kikosi chake kukumbana na kichapo kutoka kwa Levante juzi, Jumamosi.

Vinara hao wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, Barca walifungwa mabao 3-1 pale kwenye dimba la Ciutat mjini Valencia, mabao matatu yakipatikana ndani ya dakika saba za kipindi cha pili, baada ya Lionel Messi kufunga kwa penalti kipindi cha kwanza.

Hicho ni kichapo cha tatu cha Barca msimu huu na sasa wanalingana na Real Madrid kwa pointi kileleni mwa msimamo wakitofautiana mabao.

Alipoulizwa kama alishtushwa na kiwango cha wachezaji wake na kama atajiuzulu, Valverde alisema: " Sifikirii kuhusu kujiuzulu, naangalia mbele tu.

"Kila kitu kimeanguka. Hatukuanza kupindi cha pili vizuri na hatukutengeneza hatari yoyote.

"Pengine, ingawa hatukucheza vizuri na hatukutengeneza nafasi nyingi na tulijisababishia matatizo wenyewe na wakatufunga kwa urahisi.

"Bao la tatu lilikuwa rahisi zaidi kwao na kwa uhakika kabisa ilikuwa ni umakini wetu mdogo."

# Isco azigonganisha Manchester City, Arsenal

**LONDON,** England


KLABU za Arsenal na Manchester City zinamwania kiungo wa Real Madrid, Isco na zinatazamiwa kuweka ofa mezani kwa ajili ya staa huyo katika dirisha dogo la Januari.


Isco hana nafasi ya kudumu katika kikosi cha Kocha Zinedine Zidane licha ya kuwa mmoja kati ya viungo bora wachezeshaji barani Ulaya na kwa msimu wa tatu huu amekuwa akihusishwa kuondoka Santiago Bernabeu bila ya mafanikio.

Mara kadhaa imeripotiwa kuwa Isco hana maelewano mazuri na Zidane na hicho ndicho kinachomfanya kutaka kuondoka Bernabeu.

Wakati Kocha wa Arsenal, Unai Emery akipambana kuachana na Mesut Ozil mapema iwezekanavyo huku akimtamani Isco, inajulikana kuwa Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola ni shabiki mkubwa wa staa huyo wa kimataifa wa Hispania.

Na mara kadhaa Isco amehusishwa na mipango ya kutakiwa kutua Etihad, lakini mipango yote ilishindikana.



# Neymar kaikimbiza PSG kumnasa Pogba

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain waligomea ofa ya kumchukua kiungo Paul Pogba kutoka Manchester United wakati wa kipindi cha majira ya joto kilichopita, kwa mujibu wa ESPN.

Kwenye dirisha lililopita la uhamisho wa majira hayo ya kiangazi, wakala wa kiungo Pogba, Mino Raiola aliripotiwa kuwaambia PSG waende kumsajili Pogba huko Man United, lakini wababe hao wa Ufaransa hawakutaka kufanya hilo.

Kwa muda wote kwenye dirisha lililopita, Pogba alikuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Man United huku Real Madrid na Juventus zikidaiwa kuwa kwenye mchakato wa kunasa huduma yake.

Taarifa za kutoka Italia zinadai kwamba, wakala Raiola alifikia hata hatua ya kuwafuata PSG wamsajili mchezaji huyo ili tu Pogba aondoke Old Trafford, mahali ambako alikuwa na wakati mgumu alipokuwa chini ya kocha Jose Mourinho kabla ya kuachana na timu hiyo Desemba mwaka jana.

PSG wao hawakutaka kuweka nguvu kwa Pogba kwa sababu mpango wao namba moja ulikuwa kumbakiza Neymar kwenye kikosi chao na kama wangekubali ofa hiyo ya kumchukua Pogba basi kungeibuka habari za kubadilishana wachezaji, kwamba Man United nao wangehitaji huduma ya Mfaransa huyo.

Ingawa baadaye, ilionyesha kwamba, PSG walikuwa na mpango wa kumsajili ili kuziba pengo la Neymar aliyekuwa akionekana kutaka kwenda Barcelona, lakini mpango huo ukashindikana.

Hata hivyo, taarifa zaidi zinaeleza kwamba, bado PSG wanamfikiria kiungo huyo mshindi wa Kombe la Dunia.

## HABARI MICHEZO

# Mbio ubingwa Serie A ni ngumu - Sarri

**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Maurizio Sarri amesema "ni mapema" kusema kwamba, mbio za Ligi Kuu ya Italia, Serie A, ni za farasi wawili kati yao na Inter.

Ushindi wa juzi Jumamosi wa bao 1-0 dhidi ya Torino ulikifanya kikosi hicho cha kocha, Sarri kurudi kileleni mwa msimamo mbele ya wapinzani wao Inter.

Bao la Matthijs de Ligt la kipindi cha pili liliiwezesha Juve kupata ushindi huo na kuongoza kwa tofauti ya pointi moja dhidi ya Inter iliyoifunga Bologna mabao 2-1.

Hata hivyo, Sarri alikataa kukubali kwamba mbio za ubingwa wa ligi hiyo kwa sasa ni kati ya Juve na Inter, huku Atalanta wakionekana kuwakaribia kwa mbali baada ya mechi zao 11.

"Bado kuna pointi 81 tunatakiwa kuzipata. Kesho msimamo unaweza kubadilika," alisema Sarri akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa sababu ukiona msimamo wa leo (juzi) bado haujajumuisha mechi za kesho (jana Jumapili).

"Pengine Atalanta wanaweza kutukaribia kabisa. Nafikiri kwa sasa ni mapema mno kuzungumzia kuhusu ubingwa wa Ligi Kuu kwa timu mbili, bado safari ni ndefu ya kwenda."





# MAROTTA: MARTINEZ HAENDI BARCA WALA UTD

**MILAN,** Italia

OFISA mtendaji wa Inter Milan, Giuseppe Marotta amekanusha uvumi kwamba mshambuliaji wao nyota, Lautaro Martinez anakwenda kati ya Barcelona au Manchester United.

Kiwango bora cha Martinez msimu huu kimeonekana kuwavutia mabingwa wa Ligi Kuu ya Hispanaia, LaLiga, Barca na Man United ambao wapo kwenye wakati mgumu kule kwenye Ligi Kuu ya England.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 raia wa Argentina, ambaye wakala wake amezungumzia kuhusu kutakiwa na Barca, amefunga mabao saba kwa jina lake msimu huu.

Alipoulizwa kuhusu uvumi huo kwamba Barca na United zipo kwenye mbio moja ya kumwania Martinez ambaye ada yake inatajwa kuwa ni euro milioni 111, Marotta aliiambia Sky Sport Italia: "Hayo ni mazungumzo ya vyombo vya habari.

"Wachezaji wetu wana furaha kuwa na sisi na mchezaji anatakiwa kujielezea yeye mwenyewe kama anataka kuondoka. Hatuna mpango wa kuuza wachezaji muhimu, Inter ni klabu muhimu.

"Bila shaka, sehemu ya kazi ni kudili na hali kama hizi za wachezaji."

Martinez, ambaye alitua hapo akitokea Racing Club msimu wa 2018-19, amefunga mabao matano kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu huu na kufikisha mabao saba kwenye mashindano yote kwa kikosi hicho cha kocha, Antonio Conte.

Inter iliifunga Bologna mabao 2-1 juzi, Jumamosi na kuendelea kukimbizana na mabingwa watetezi Juventus ambao wamewapita pointi moja, baada ya michezo 11 ya ligi hiyo.

# *'Vigumu Liver kuepuka kichapo'*

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesisitiza kwamba kwenda msimu mzima bila kufungwa si rahisi kwa Liverpool, hasa wakicheza kama walivyopata ushindi wa dakika za majeruhi dhidi ya Aston Villa juzi, Jumamosi.

Bao la Sadio Mane la dakika za majeruhi na lile la Andy Robertson liliwafanya waibuke na ushindi wa 2-1 dhidi ya Villa na kuifanya Liverpool kuendeleza rekodi ya kutofungwa hadi sasa.

Liverpool imebaki na pointi sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu wakati wakielekea kwenye mchezo dhidi ya Manchester City pale kwenye dimba la Anfield.

Alipoulizwa kama Liverpool wanaweza kumaliza msimu wote bila kufungwa wakiwa wamefikisha pointi 28, Klopp alisema, si rahisi, hasa wakicheza kama juzi Jumamosi.

Aliiambia Sky Sports: "Si rahisi kama unacheza kama tulivyocheza Jumamosi. Haikuwa mbaya, tulicheza vizuri, lakini mchezo haukuwa na hamasa ya ushindi.

"Pengine haiwezekani, lakini hatufikirii kuhusu hilo kwa sasa. Tunafikiri namna gani tunashinda mchezo unaofuata."


"Bado tunachakujifunza na kujiimarisha na muda mwingine tunatakiwa kupigana hasa. Tukifanya makosa tunaweza kupoteza mchezo.

"Hatukustaili kushinda kwa aina ile, nimeridhishwa na matokeo, lakini kulikuwa na wakati sikupenda."

Liverpool sasa itacheza na Genk Jumanne kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, kabla ya kuwavaa wapinzani wao Manchester City Jumapili ijayo.



# DOND… A SOKA MAGA… ULAYA




# GUARDIOLA AMSHUKIA MANE AKIJIHAMI LIVER

●●● Muda mwingine yeye anajirusha, wakati mwingine anaonyesha kipaji chake kwa kufunga...

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola 'amekoleza' moto wa mechi yao dhidi ya Liverpool wikendi ijayo kwa kumshutumu Sadio Mane kwa kujirusha.

**Liverpool ambao ni vinara wa Ligi Kuu ya England wameizidi Man City pointi sita wakati wakielekea kwenye mchezo baina yao wa Ligi Kuu utakaopigwa pale Merseyside Jumapili ya Novemba 10, mwaka huu.**

Timu zote, City na Liverpool zilipata ushindi kwenye mechi zao za Jumamosi, huku kikosi cha Jurgen Klopp kikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya wageni wao Aston Villa shukrani kwa bao la ushindi la Mane la dakika ya mwisho.

Timu hizo mbili katikati ya wiki hii zitakuwa kwenye majukumu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kabla ya kukutana wikendi ijayo pale kwenye dimba la Anfield.

Hata hivyo, Guardiola ametupa shutuma kwa wapinzani wake hao akimshutumu mshambuliaji raia wa Senegal, Mane kwa kudai kwamba alijaribu kumdanganya mwamuzi wakati alipoonyeshwa kadi ya njano kwa kujirusha pale kwenye Uwanja wa Villa Park, juzi Jumamosi.

"Muda mwingine yeye (Mane) anajirusha," alisema Guardiola akiiambia Sky Sports.

"Wakati mwingine anaonyesha kipaji chake kwa kufunga mabao ya kuvutia dakika ya mwisho. Ana kipaji."

Ushindi wa Liverpool ulikuja kwa bao utata la Andrew Robertson na Mane akafunga la ushindi dakika 87.

Guardiola anatambua kwamba, hakuna kitu kinachoitwa bahati kwenye timu ya Klopp, kwani kupambana ndio kunakoleta matokeo uwanjani katika mechi zote.

Aliongeza: "Kukaribia ushindi mwingine kwa Liverpool? Kama mara moja, mbili, tulikuwa na bahati, tulikuwa na bahati.

"Lakini ilitokea mara nyingi kwenye misimu miwili iliyopita, mara nyingi. Wana utamaduni maalumu wa kufanya hivyo. "Tunajiandaa sisi wenyewe, tunajua timu gani tunapambana nayo, nafikiri wanaweza kushinda mechi 10 na kutoka sare moja.

"Wiki ijayo tunakwenda Anfield kucheza dhidi yao."

## ZISIKUPITE

### WERNER VITANI CITY, UNITED

MANCHESTER United ipo tayari kuipiku Liverpool, mchakato wa kumsajili straika wa Leipzig, Timo Werner, 23. ***(Mirror)***

### ONANA AIVUTIA TOTTENHAM

TOTTENHAM inazingatia uwezekano wa kumfuata kipa wa Ajax na Cameroon, Andre Onana, 24, anayetajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 35. ***(Sun)***

### BAYERN BADO INAYE SANE

BAYERN Munich bado ipo tayari kumsajili winga wa Manchester City, Leroy Sane, lakini itatoa ofa ya pauni milioni 69 pekee Mjerumani huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Calciomercato)***

### IBRAHIMOVIC AHUSISHWA UTD

MSHAMBULIAJI wa Msweden Zlatan Ibrahimovic, 38, ambaye kwa sasa anacheza Ligi Kuu ya Marekani (MLS) katika klabu ya LA Galaxy, lakini amehusishwa na kurudi Manchester United, ila anaweza kurudi klabu yake nyingine ya zamani ya AC Milan. ***(Marca)***

### MILAN KUACHANA NA EVERTON

AC Milan inatarajiwa kuhitimisha lengo lao la kumsajili mshambuliaji wa Gremio, Mbrazil Everton Soares, 23, ambaye amekuwa akihusishwa na Tottenham. ***(Calciomercato)***

### WEST HAM KUMUUZA SANCHEZ

WEST Ham inajiandaa kumuuza kiungo Mcolombia Carlos Sanchez, 33, kwa pauni milioni 3.5 kwenye dirisha la usajili la Januari. ***(Football Insider)***

### SOLSKJAER ASHTUKA UBUTU

OLE Gunnar Solskjaer amesema Manchester United lazima itafute suluhisho la ndani la ufungaji mabao kufuatia kuchapwa 1-0 na Bournemouth. ***(Manchester Evening News)***

### APOTEZEA HATIMA YAKE

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery amepotezea swali kuhusu mustakabali wake wa baadaye kufuatia timu hiyo kutoka sare nyumbani dhidi ya Wolves. ***(Express)***

### WAMFUATILIA RYAN

WASAKA vipaji wa Newcastle, walikuwapo Uwanja wa Elland Road Jumamosi kumtazama kiungo wa QPR na Jamhuri ya Ireland, Ryan Manning, 23. ***(Football Insider)***

### BARCA KUMRUHUSU ALENA

BARCELONA itamruhusu kiungo wa Mhispania Carles Alena, 21, anayeaminika kuwindwa na Tottenham, kuondoka klabuni hapo dirisha la usajili la Januari. ***(Mundo Deportivo, via Mail)***

### POCHETTINO APOTEZEA USAJILI

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino anajaribu kutafuta fomula mpya kuiwezesha timu yake kusonga mbele na haifadhi fedha kwa ajili ya kuwasajili Tanguy Ndombele, 22, Giovani Lo Celso, 23, na Ryan Sessegnon, 19, katika majira ya joto ili kutoa suluhisho la haraka. ***(Sky Sports)***

## Kili Marathon yazinduliwa rasmi

**Na Mwandishi Wetu**

MBIO maarufu za Kilimanjaro Premium Lager Marathon za 18 zimezinduliwa rasmi jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe huku akitoa wito kwa Watanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki hapo Machi Mosi mwakani.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo jijini Dar es Salaam, Waziri Mwakyembe amewapongeza wadhamini wa Kilimanjaro Marathon wakiongozwa na Kilimanjaro Premium Lager wanaodhamini Km. 42, Tigo Km. 21 na Grand Malt Km. tano kwa kudhamiria kukuza sekta ya michezo hususan riadha na kufanya mbio hizo kuwa kubwa mwaka hadi mwaka.

"Inatia moyo sana kuona kuwa Kilimanjaro Marathon sasa hivi ina washiriki zaidi ya 11,000 kutoka nchi zaidi ya 56 kote duniani. Hili ni jambo zuri sana kwa taifa kwani tunapata fedha za kigeni kutokana na matumizi yanayofanywa na wageni hawa nchini ikiwamo utalii ambao sasa hivi tuna kitu kinachojulikana kama 'sports tourism'," alisema huku akitoa changamoto kwa Watanzania pia wachangamkie fursa ya kufanya utalii wa ndani baada ya mashindano hayo.

## Ndalichako ahimiza michezo Elimu ya Juu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amewataka watumishi wa Taasisi za Elimu ya Juu nchini kushiriki michezo na kufanya mazoezi kila Jumamosi ya pili ya kila mwezi kwa ajili ya kujenga miili yao kiafya ili kujiepusha na magonjwa yasiyoambukiza.

Aidha, alisema kushiriki kwao katika michezo mbalimbali pia kutasaidia kuzalisha wanamichezo bora watakaoweza kushiriki katika mashindano mbalimbali ya Taasisi za Elimu ya Juu na mingineyo.

Prof. Ndalichako alisema hayo katika hotuba yake wakati wa kufunga mashindano ya Chibunda CUP 2019/2020 katika viwanja vya Kampasi Kuu - SUA. Waziri Ndalichako alisema, serikali ya awamu ya tano inahimiza michezo na mazoezi na imetenga Jumamosi ya pili kila mwezi wananchi kufanya mazoezi ili kujiepusha na magonjwa yasiyoambukiza.

Prof. Ndalichako aliupongeza uongozi wa Chuo Kikuu SUA chini ya Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Raphael Chibunda kwa kuanzisha mashindano ya Chibunda Cup ikiwa na lengo la kujenga kiwanja cha kisasa cha mchezo wa Kikapu.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu hicho, alisema, chuo kimetenga muda kwa ajili ya shughuli za michezo ya aina mbalimbali kwa wafanyakazi wa idara zake kushindana na washindi kupatiwa zawadi mbalimbali za medali na vikombe.

# MOROCCO: ZANZIBAR HEROES YA CECAFA HADHARANI J'MOSI

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha kwanza cha wachezaji watakaounda timu ya Soka ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), ambacho kitashiriki mashindano ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati kinatarajiwa kutangazwa Jumamosi wiki hii, imeelezwa.

**Mashindano ya Kombe la Chalenji yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), yanatarajiwa kufanyika kuanzia Desemba Mosi hadi 19, mwaka huu jijini Kampala, Uganda na tayari nchi 11 zimethibitisha kushiriki michuano hiyo.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zanzibar Heroes, Hemed Morocco, alisema kikosi hicho cha awali ambacho kitakuwa na wachezaji wanaoshiriki Ligi Kuu Zanzibar kitaanza mazoezi Novemba 10, mwaka huu Kisiwani Unguja.

Morocco alisema baadaye nyota hao watafanyiwa mchujo na watakaobaki wataungana na nyota wengine wanaocheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ajili ya kupata kikosi kamili kitakachopeperusha bendera ya Zanzibar katika mashindano hayo.

"Uteuzi wa kwanza wa timu yangu utafanyika Novemba 9, baadaye Ligi Kuu Tanzania Bara itakaposimama Novemba 24, nitakuwa nimepata wachezaji wengine ambao wataungana na nyota watakaobakia katika mchujo wa kule Zanzibar na kukamilisha kikosi," alisema Morocco.



Kocha huyo aliongeza kuwa anaamini kikosi chake kitajiandaa kwenda kupambana na hatimaye kurejea na ubingwa wa michuano hiyo kwa sababu uwezo na uzoefu wanao.

"Tunataka kwenda kumalizia kazi tuliyoiacha mwaka juzi, tutajiandaa vizuri kwa sababu tunajua mashindano yale ni magumu, mechi zote zina ushindani," Morocco alisema.

Katika mashindano hayo yaliyopita ambayo yalifanyika Kenya katika miji ya Machakos, Kisumu na Kakamega, Zanzibar Heroes ilifungwa mabao 2-1 na wenyeji Harambee Stars kwenye mchezo wa fainali mbele ya Makamu wa Rais wa nchi hiyo, William Ruto.



Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro (kushoto), akipokea zawadi ya kushiriki katika mashindano ya kwanza ya gofu ya mabalozi kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Wateja Rejareja Maalum wa Benki ya NBC, Ashura Waziri, yaliyofanyika katika viwanja vya gofu vya Sea Cliff Kisiwani Zanzibar mwishoni mwa wiki. Mashindano hayo yalidhaminiwa na NBC ikiwa ni sehemu ya shughuli za kusapoti sekta za michezo na utalii nchini. **NA MPIGAPICHA WETU**

# NBC kuzidi kuibeba gofu Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kudhamini mashindano ya kwanza ya gofu ya mabalozi visiwani Zanzibar kwa mafanikio makubwa, Benki ya NBC imeahidi kuendelea kusapoti sekta ya michezo na utalii visiwani humo kutokana na mchango wake mkubwa katika maendeleo ya taifa.

Akizungumza wakati wa mashindano hayo katika viwanja vya Gofu vya Sea Cliff visiwani humo mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Rejareja Maalum wa Benki ya NBC, Ashura Waziri, alisema licha ya kwamba michezo husaidia kuimarisha afya kitu ambacho ni muhimu katika uzalishaji mali, lakini pia inaweza kuongeza ajira na kuinua uchumi wa wanamichezo na taifa.

"Naihakikishia Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar kwa kupitia Kamisheni ya Utalii, kuwa NBC itaendelea kuisaidia kwenye michezo kama tulivyofanya kwa kudhamini gofu ya mabalozi, tunathamini michezo kwa wafanyakazi wetu pia, tunaihakikishia Wizara ya Michezo pia tutaendelea kusapoti michezo," alisema.

Naye Meneja wa Tawi la NBC mjini Zanzibar, Ramadhani Lesso, alisema NBC imekuwa mdau mkubwa wa maendeleo visiwani humo na ndio sababu ya kuitikia wito wa Wizara ya Habari na Utalii kupitia Kamisheni ya Utalii kushiriki katika mashindano hayo kwani wamekuwa wakishirikiana kwa muda mrefu katika kusapoti utalii visiwani humo.

"Kama mnavyofahamu benki yetu ina ATM zisizopungua saba hapa Zanzibar na zote zinatoa huduma ya Visa ambayo ni maalumu kwa ajili ya wananchi wote, lakini zaidi kwa watalii. Kwa hiyo utakuta watalii wanafaidika sana wanapotumia mashine zetu za kutolea pesa na mashine nyingine zilizopo kwenye hoteli.

"Watalii ni muhimu sana kwetu ndio maana tulipopata mwaliko huu kutoka kwa Mkurugenzi wa Kamisheni ya Utalii tuliona ni sehemu muhimu sana kwetu kwa ajili ya kuunga mkono serikali kwa upande wa maendeleo na vilevile ikiwa ni sehemu ya michezo kama ilivyo sera ya michezo," aliongeza.

Pamoja na hayo meneja huyo akatoa wito kwa serikali na wadau wa michezo kuunga mkono juhudi za kusapoti mchezo wa gofu ufundishwe shuleni na sehemu zote ili Watanzania wote waweze kuucheza na kuupenda.

Katika mashindano hayo, ambayo mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Damas Ndumbaro, ambaye pia alikuwa mshiriki wa mchezo huo, Eliah John aliibuka kidedea kwa kushika nafasi ya kwanza huku Issa Mohamed Chaap wote wa visiwani humo akishika nafasi ya pili.